IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 1

Jan – Feb – Machi
2024

# HabariNjema
## KILA SIKU

**BURE**
HALIUZWI
CHAPISHO HILI LIMELIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI LISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO NCHI YA MBALI. (MITHALI 25:25).

Uebert & BeBe
ANGEL




## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma, Uebert na BeBe Angel ni watangulizi na sauti zinazoongoza katika kutangaza Habari Njema ya neema ya Mungu (Euaggelion) na unabii duniani kote. Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu vinavyouza sana kama vile Spiritual Warfare, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural Power of The Believer, n.k. Uebert na BeBe Angel ni wazungumzaji wa mikutano wanaotafutwa sana kimataifa na kama viongozi wa kimataifa, wanaheshimiwa sana kwa maono yao, ubunifu, na ujasiri. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News Church (Spirit Embassy) na wanaokalia ofisi ya kinabii wameathiri maisha ya mamilioni ulimwenguni kote kupitia shauku yao ya kuvuna nafsi kwa kuleta ufunuo wa Habari Njema ya neema ya Mungu (Euaggelion).

# HERI YA MWAKA MPYA WA MAZIWA NA ASALI



**Ufunuo 1:8**
**Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi**

Watu wengi wanaposikia maneno yaliyo hapo juu, ambayo ni ya kawaida katika jumuiya za Kikristo, wanaelekea kufikiri kwamba Mungu ndiye mwanzo na mwisho. Huo ndio uelewa wa jumla wa maandiko, ilhali kuna jambo la ndani zaidi lililopachikwa katika maneno hapo juu. Sasa hivi unaweza kuwa unajiuliza, "Mtu wa Mungu anamaanisha nini hasa?" Kaa nami.

Alfa na omega kwa hakika humaanisha "Yule anayeanza na mwisho kabla ya mwanzo." Biblia inasema Kristo alisulubishwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, maana yake mwisho ulikamilika kabla hajazaliwa na Mariamu. Mungu alikamilisha kila kitu kuhusu wewe, na ulibarikiwa na baraka zote za kimwili na za rohoni.

Dola milioni unazotafuta ziliwasilishwa tayari; afya yako ni wakati uliopita mbele yake. Dai mali yako leo unapofanya maagizo na matamko ya kiroho. Mungu alikupa kifurushi kilichokamilika, na hakuna kinachokosekana au kupungua kwa Jina la Yesu. Utafurahia maziwa na asali tu mwaka huu katika Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimebarikiwa kwa baraka zote za kiroho; maisha yangu yamekamilika. Sitapungukiwa na kitu chochote kizuri au chochote kinachohusu maisha kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 46:10

**Je, uko tayari kuanza mkakati wako wa siku 365 za kusoma Biblia?**
**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 1-3



**Matendo 9:3**
**Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafla ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni.**

Maisha ni matokeo ya mtembeleo, iwe ya kiungu au ya kishetani. Mtembeleo wa kiroho huja kwa namna ya Mungu kuzungumza nawe moja kwa moja, mtu anayekutana nawe, au aina yoyote ya tukio muhimu. Mtume Paulo alikutana nao njiani kuelekea Dameski. Alipigwa na mwanga wa ajabu, ambao baadaye ulimfanya awe mtume mkuu wa wakati wote kiasi kwamba hata Petro aliguswa na baadhi ya maandishi yake. Ujumbe wa maandishi kutoka kwa Paulo yalichukuliwa kuwa maandiko kwa sababu ya mtembeleo wake mwenyewe.

Unaposoma habari hii leo, inaweza kuwa mtembeleo wako mwenyewe wa kubadilisha vizazi na historia katika familia yako. Mtembeleo wako unaweza kuwa mtu ambaye unakutana naye leo. Tumia kila mtembeleo mzuri kutangaza ushindi wako juu ya adui. Una mtembeleo kupitia neno hili, na hakika utatoka na kufanya matokeo yanayoonekana.

## UKIRI WA KINABII

**Nina mtembeleo binafsi kupitia neno la leo, na hakuna kitakachonizuia kufurahia maziwa na asali mwaka huu kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 4-7



**Ayubu 22:28**
**Nawe utakusudia neno, nalo litathibitika kwako, na mwanga utaziangazia njia zako.**

Kila neno linalotoka kinywani mwako linafanya kazi na linangojea kutimizwa. Ndio maana ni muhimu kuweka viwango kwa maneno unayotamka kutoka kwenye midomo yako. Kumbuka, Biblia hata inasema mauti na uzima vipo katika uwezo wa ulimi wako. Haimaanishi baadhi ya magonjwa au kushindwa kwa madaktari bali maneno yako mwenyewe. Weka thamani kwenye maneno unayozungumza.

Wakati unaposema "mambo ni magumu, "neno hilo linangojea kufanya kila kitu kiwe kigumu kwako. Litasubiri hadi itimie. Njia pekee ya kufuta maneno hasi ni kwa kuzungumza maneno chanya. Ongea maneno chanya kwenye hali yako, na utaishi kulingana na maneno yale yale unayozungumza.

Hii ni siku mpya; lugha yako ni ya kujenga tu, si kuharibu. Hata kama mashinikizo ya maisha yanakusonga, dumisha lugha yako chanya. Wewe ni mbarikiwa wa Aliye Juu, na hakuna umaskini au ugonjwa utakaokaribia hema yako kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Kinywa changu ni kalamu ya mwandishi stadi; Natamka maziwa na asali katika duru zote za maisha yangu. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu katika Jina la Yesu. Utukufu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 18:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 8-11



**Zaburi 92:12-13**
**Mwenye haki atasitawi kama mtende, atakua kama mwerezi wa Lebanoni Waliopandwa katika nyumba ya Bwana watasitawi katika nyua za Mungu wetu.**

Lebanoni ni mbaya sana linapokuja suala la hali ya hewa yake. Wakati mwingine pepo kali, zenye dhoruba zinapita katika upana wa nchi na kusababisha uharibifu mkubwa kwa majengo na miti. Wengi watajiuliza ni nini kinatokea kwa mtende wa Lebanoni hata kusababisha mtunga-zaburi kufananisha mwenye haki na mtende wa Lebanoni.

Pepo zikivuma, mtende wa Lebanoni utainama tu na kurudi mahali pake. Unainama si kwa sababu ni dhaifu lakini kwa sababu unajipinda. Kristo alikufanya kuwa mwenye haki wa Mungu na mwenye haki ni kama mtende wa Lebanoni. Ikiwa wanazungumza au kuandika mabaya dhidi yako, utainama tu na kurudi kwenye msimamo wako. Hutatikiswa wala kung'olewa na kitu chochote. Wewe ni mwenye nguvu na mwenye kujipinda kama mtende wa Lebanoni, na msingi wako ni wenye nguvu kuliko shinikizo la maisha.

## UKIRI WA KINABII

**Nina nguvu na imara katika Yesu Kristo. Hakuna silaha itakayofanywa dhidi yangu itakayofanikiwa. Nilizaliwa kushinda na kufanikiwa kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi1:3-4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 1-5



**Mathayo 11:11**
**Amin, nawaambieni, Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye.**

Andiko letu liko wazi kwamba kwa wale wote waliokuja kabla ya Yohana, hapakuwa na mkuu zaidi yake. Huenda akawa Isaya, Yoshua au mtu ye yote unayeweza kumfikiria; hakuna aliyepewa neema kama Yohana. Alikuwa akifanya kazi katika kiwango chake cha pekee cha neema na nguvu. Kwa kushangaza, Yesu aliendelea kusema kwamba hata aliye mdogo kabisa miongoni mwa Wakristo waliozaliwa mara ya pili ni mkuu kuliko Yohana.

Ndugu na dada, Yohana alifanya maajabu, lakini tunaweza kufanya maajabu bila hesabu. Toka kwa ujasiri huu kwamba wewe ni jenerali wa nyota tano wa Mungu, na unaweza kubadilisha mambo katika maisha yako. Nena maneno na utabiri anga, na mazingira yako yatakubali neno lako.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni jemadari wa nyota tano niliyezaliwa kwa Roho wa Mungu. Ninaamuru na kutangaza kwamba maisha yangu ni zaidi ya maajabu. Hatua zangu zinaongozwa na Mungu katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 14:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 6-9



**Yakobo 4:7**
**Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.**

Neno shetani si jina tu bali ni maelezo ya kazi ambayo yanaeleza mtu anayeshambulia na kushambulia mpaka atoboe. Alichoshinda shetani ni uthabiti katika harakati zake za kukushinda. Hata alimwacha Yesu kwa muda baada ya kumjaribu, ambayo ina maana kwamba alikuwa akirudi kwa msimu mwingine. Ingawa Yesu alikuwa Mungu katika mwili, adui bado alikuwa na ujasiri wa kushambulia na kushambulia.

Unapojilisha kwa Neno na kuweka ubora kwenye maneno unayosema, omba katika Roho Mtakatifu. Utajenga upinzani dhidi ya adui. Utaunda stamina dhidi ya mishale yote ya adui na uhalisia wa maziwa na asali utakuwa wako. Chukua muda wa kuliendea Neno, ukiomba katika Roho Mtakatifu, na hakika utarudi na ushuhuda. Utaishi maisha ya ushindi wa uhakika dhidi ya adui.

## UKIRI WA KINABII

**Ninajijenga katika imani takatifu zaidi kwa Neno na maombi. Kinywa changu kinatoa uzima, amani na mafanikio katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yuda 1:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 10-13



**Mwanzo 1:3**
**Na Mungu akasema; Iwe nuru; na ikawa nuru.**

Kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, Mungu alifanya jambo moja tu: Alisema! Hakuna chochote cha kimwili, lakini kinywa chake kiliumba dunia, kilishinda kuta na kubadilisha maisha ya watu wengi. Mambo yale ambayo yanaonekana kimwili machoni pako, ukichunguza kwa undani zaidi, utagundua kwamba alisema neno moja tu na ikawa. Ndio maana Mungu anathamini unabii kwa sababu ofisi ya unabii inatamka tu.

Mungu alipoona giza katika kitabu cha Mwanzo, hakulalamika bali alitamka nuru ikawa. Leo, tumia kinywa chako kwa faida kwa kusema kiwe chochote unachotamani. Je, ni pesa, kazi, mikataba, ukuaji, au ndoa? "Nena tu, nayo itathibitika.

## UKIRI WA KINABII

**Nilichagua kutumia kinywa changu kwa faida na ninaunda himaya kwa ulimi wangu. Ninaamuru na kutangaza maziwa na asali katika maisha yangu kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 12:36

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 14-16



**1 Timotheo 1:18**
**Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri;**

Unabii si usemi tu wa maneno ya Ki-Mungu bali ni kuachiliwa kwa silaha. Paulo alimuagiza Timotheo atumie unabii wake mwenyewe kupigana vita vizuri. Hakumwambia atumie miunganiko yake, wasifu au faida yoyote ya kimwili, bali unabii. Neno la kinabii linapoachiliwa juu yako kupitia neno lililohubiriwa, maandiko, au kukutana na mtu mmoja-mmoja, ni silaha uliyopewa. Tayari umeandaliwa na neno hilo.

Chimbua kwa kina kila neno chanya ulilopewa na usimame juu ya neno hilo ili kupigana vita dhidi ya adui. Ikiwa uliambiwa kuwa utakuwa mkombozi wa familia yako, basi adui hawezi kukuzuia au kuacha maendeleo yako kwa sababu unabeba kazi ya kizazi cha kutoa familia nzima. Nenda nje na ushinde katika mikondo yote ya maisha yako. Hakuna kitakachokuzuia kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mbeba neno la kinabii la Mungu. Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Sitashindwa na adui wala changamoto yoyote. Msingi wangu ni mgumu na imara katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Kumbukumbu la Torati 31:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 17-20



**Yoeli 3:10**
**Yafueni majembe yenu yawe panga, na miundu yenu iwe mikuki; aliye dhaifu na aseme, Mimi ni hodari.**

Ukipunguzwa hadi kwenye sehemu yake ya msingi, utagundua kuwa imani si chochote zaidi ya hoja. Adui atakuwa anajaribu kukusukuma kwa njia yake mwenyewe, na jukumu lako ni kupinga mpango wa adui. Biblia iko wazi kwamba unapomtii Mungu na kumpinga shetani, atakimbia.

Maandiko yetu ya leo yanasema walio dhaifu na waseme mimi nina nguvu. Zingatia, wadhaifu hawasemi wao ni wahodari wakipata nguvu lakini wakati wakiwa bado ni dhaifu. Wanajua mambo ya hakika yanasema kwamba wao ni dhaifu, si matajiri, au wagonjwa, lakini wanapaswa kuchagua kubishana na hali hizo. Leo, fanya mabishano dhidi ya mipango yote ya matukio mabaya katika maisha yako. Ikiwa akaunti yako ya benki ni tupu, sema tu, "Pesa zinakuja katika mwaka huu wa maziwa na asali!" na itakuwa hivyo. Usiikubali hali yoyote inayotoka kwa adui; ipinge kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa kutoka juu, na chanzo changu ni cha Ki-Mungu. Nimebarikiwa kupita kiasi, na nguvu za Mungu zitadhihirika katika biashara yangu, afya yangu na maeneo yote ya maisha yangu katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2Wakorintho 4:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 21-23



**Mathayo 8:27**
**Lakini wale watu wakatahamaki, wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii?**

Baba yangu, Mchungaji Chris Oyakhilome, alinitetea wengi waliponikosoa kuhusu pesa za miujiza. Ilikuwa nje ya ufahamu wa watu wengi kuamini kuwa pesa zinaweza kunyesha pesa za kawaida na za mtandaoni kwa mamilioni. Kama vile hata Yesu alivyofanya pesa za miujiza, ambazo Biblia yako mwenyewe iliziita "pesa ya kodi ya miujiza," wengi bado hawaamini kwamba katika siku hizi na zama hizi, Mungu bado yuko katika biashara ya kufanya pesa zionekane. Katika maandiko yetu hapo juu, hawakuweza kuelewa Yesu alikuwa mtu wa namna gani kwa sababu alikuwa na siri za kudhibiti bahari na dhoruba.

Mchungaji Chris alisema wale wote waliokuwa wakihoji kuhusu pesa za miujiza hawakuelewa "siri. " Kuna kanuni za kiroho, kaka na dada, ambazo zinakufanya uingie katika ulimwengu wa miujiza ambayo wengine hawapati. Ni kama kuandika programu za kompyuta; tunaingiza mistari yote ya alama, na miujiza itatokea. Leo utapata miujiza ya ajabu kwa Jina la Yesu. Neno hili, pamoja na maombi yako, litakuzindua katika ulimwengu wa alama za Kimbinguni ambazo zitasababisha miujiza juu ya miujiza!

## UKIRI WA KINABII

**Nimejaa Neno, na roho yangu iko makini . Ninaishi katika ulimwengu tofauti wa nguvu. Shughuli zisizo za kawaida zitaendelea kutokea katika maisha yangu kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 2:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 24-28



**Matendo 9:3**
**Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni.**

Maombi ni itifaki au muhudumu unayemtuma mbele yako kutekeleza kazi fulani. Kwa wengine, huenda ikasikika kama kubwabwaja maneno tu, lakini maombi ni chombo chenye nguvu cha kuunda wakati ujao unaotamani. Anania alikuwa mfuasi fulani tu, lakini maombi yake yalilijaza anga la Dameski kiasi kwamba Paulo alipoelekea Dameski, alipigwa na radi. Ingawa Anania alikuwa mfuasi fulani tu, maombi yake yaliwekwa kwenye anga ili kunasa vitisho vyote dhidi ya misheni ya Mungu. Maombi yake yalikuwa kazini, kama mtu wa itifaki au muhudumu katika anga.

Omba maombi yako bila kukoma, na kila neno utakalotangaza litathibitika. Nena maziwa na asali ambavyo ni mafanikio, maisha marefu, afya na kuinuliwa, na vitathibika kwa Jina la Yesu. Tuma mtu wa itifaki wako kwenye viwanda na maeneo yote ambayo hayajatekwa. Wewe si dhaifu kama unaweza kuomba. Tumia wakati huu kumpa jukumu muitifaki wako, na ushindi ni hakika.

## UKIRI WA KINABII

**Wakati ujao ni wangu, na hakuna kitakachonizuia kufanikiwa. Maombi yangu yapo kazini; hakika yatakamilisha kazi zake zote katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 29-31



**Zaburi 119:130**
**Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga.**

Namna kuu ya ukombozi ni pale ujinga wako unapokabiliwa. Biblia inapomwita shetani mkuu wa giza, sivyo watu wengi wanavyofikiri. 'Mkuu' hapa maana 'kwanza', na giza maana yake ni 'ujinga,' kwa hiyo inamaanisha yeye ni mtu wa kwanza kuwa mjinga. Alipofikiria kufanya mapinduzi Mbinguni, akawa namba moja kwenye orodha ya wajinga.

Kuna yale maeneo ambayo umekuwa huyajui; hizo ni sehemu zile zile ambazo shetani na wenzake hufanikiwa zaidi. Acha Neno hili la Mungu liangaze katika kila eneo la maisha yako. Zingatia maeneo yote ambayo ulikuwa unafeli. Kufafanusha kwa Neno la Mungu kutaleta nuru, na utabadilishwa kwa kufanywa upya nia yako.

## UKIRI WA KINABII

**Akili yangu inafanywa upya kwa Neno la Mungu. Kristo ndani yangu ndiye tumaini la utukufu wote. Mimi ni mfano wa nuru, na mafanikio hakika ni yangu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 3:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 32-34



**Zaburi 138:2 (NEN)**
**Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa kuwa umelikuza jina lako na neno lako juu ya vitu vyote.**

Unapoliendea Neno, hakika utarudi na ushuhuda. Huduma yetu inajulikana hasa kwa ufunuo wa Neno kuliko kitu chochote. Hata kama tunatabiri na kufanya kazi katika karama zingine za kiroho, bado tunasisitiza Neno la Mungu, ambalo ni neno la uhakika zaidi la unabii. Kulingana na andiko hilo hapo juu, Mungu hata ameliinua Neno Lake kuliko jina Lake. Kwa kweli, Yeye hutafuta shauri kenye Neno Lake kabla ya kufanya lolote. Ndio maana Neno la Bwana ni kipimo kwa kila kitu kinachotokea hapa duniani.

Kila kitu ni matokeo ya Neno la Mungu, na kadiri unavyozama ndani ya Neno katika Neno la Mungu, ndivyo utakavyopata masuluhisho zaidi. Tengeneza muda wa kusoma na kusikiliza Neno la Mungu, na hakika utarudi na ushuhuda. Kamwe usijiepushe na Neno la Mungu; ni neno la unabii lililo hakika zaidi.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaliendea Neno la Mungu, ambalo ni neno la uhakika la unabii kwa maisha yangu, afya na biashara yangu. Maisha yangu ni mfano halisi wa Neno la Mungu, na ninaishi kulingana na mapenzi ya Mungu katika Jina la Yesu**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 55:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 35-37



**Luka 16:13**
**Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana ama atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu, Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.**

Kuna jambo moja tu katika Biblia ambalo Mungu alijiweka sawa nalo. Chombo kimoja tu ambacho Mungu Mwenyewe alithibitisha kwamba hiki kinaweza kunipa ushindani kamili, na sio shetani bali ni PESA. Pesa ni bwana; inatafuta kudhibiti na kuabudiwa. Inapokuona, huona mtu wa kudhibitiwa na kutawaliwa. Kulingana na maandiko, Mungu hata aliiita bwana, na anathibitisha kwamba huwezi kumtumikia Yeye na pesa kwa wakati mmoja.

Unapobobea katika ustadi wa kuzidhibiti pesa, unaweza kumtumikia Mungu kwa urahisi. Unaidhibitije pesa? Kila wakati unapotoa pesa kwa Mungu au kwenye misheni yake, uniambia pesa kwamba kuna Bwana mkuu juu yako, na kwa kufanya hivyo unaidhibiti pesa. Kutoa pesa ndio njia pekee ya kuitawala pesa. Huduma yoyote ambayo unaweza kuwa sehemu yake, usisite kutoa pesa, kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kuidhibiti pesa, na nyingi zaidi zitakujia katika mikondo tofauti.

## UKIRI WA KINABII

**Nina udhibiti wa kifedha na ustadi juu ya pesa. Sitafilisika siku yoyote katika maisha yangu na nitafurahia maziwa na asali mwaka huu. Pesa yangu ni pesa yenye misheni. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Hagai 2:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 38-39



**Luka 8:2-3**
**Na wanawake kadha wa kadha ambao walikuwa na pepo wabaya na magonjwa wakaponywa, nao ni Mariamu aitwaye Magdalene, aliyetokwa na pepo saba, na Yoana mkewe Kuza, wakili wake Herode, na Suzana, na wengine wengi, waliokuwa wakimhudumia kwa mali zao. .**

Injili ni bure kabisa, lakini njia ya kuileta kwa watu si bure. Inachukua pesa kukodi uwanja wa michezo kwa ajili ya injili, kuchapisha matoleo haya , ingawa tunayatoa bila malipo au kununua mifumo ya matangazo ya umma ili kuhubiri Injili kwa mamilioni ya watu. Hii ndiyo sababu kuu kwa nini Mungu anataka kukupa pesa, ambayo sio pesa tu bali ni pesa yenye utume. Ni pesa kwa ajili Yake.

Pesa zinakuja kwako kama nilivyotabiri, lakini kumbuka, hazipo ili kuzima tamaa zako binafsi bali kwa ajili ya utume wa Mungu. Ni kwa ajili ya kazi ya Mungu kupelekwa mbele. Unaposoma chapisho hili la ibada, neema inapatikana kukufanya uwe tajiri, lakini kumbuka kwamba fedha zinakuja si kwa ajili yako tu bali pia kwa ajili ya misheni ya Mungu. Kama wale wanawake waliomtumikia Yesu kwa mali zao, kwa kuongezeka kwako, mataifa yatapokea Injili.

## UKIRI WA KINABII

**Pesa inakuja kwangu, na sio pesa tu bali pesa yenye misheni. Ninaomba na kutabiri kwamba sitakosa rasilimali au pesa kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 2:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Ayubu 40-42



**2 Wakorintho 5:17**
**Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama, Yamekuwa mapya.**

Kwa wewe tu kuwa ndani ya Kristo, Biblia inasema wewe sasa ni kiumbe kipya. Neno ' mpya ' ni neno la Kiyunani kainós, ambalo maana yake ni ' kiumbe ambacho hakijawahi kuwepo kabla ya.' Hujawahi kuwepo hapo awali. Wanapojaribu kukukumbusha juu ya udhaifu wako wa zamani na kushindwa, wajulishe tu kwamba haujawahi kuwepo hapo awali. Wewe ni kiumbe kipya kabisa juu ya uso wa dunia. Haleluya!

Unaposoma neno hili, mambo yote yamekuwa mapya. Usiruhusu ulimwengu ukukumbushe ya zamani au udhaifu wako kwa sababu wewe ni spishi mpya kabisa ambayo haijawahi kuwepo hapo awali. Kushindwa na kushindwa sio sehemu yako maana wewe ni kiumbe kipya mwenye vinasaba vya Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya. Hakuna nguvu ya Kuzimu inayoweza kunizuia kwa Jina la Yesu. Utukufu ni kwa Mungu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 3:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 12-15



**2 Wafalme 6:17**
**Elisha akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona, na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote.**

Vitongoji vimegawanywa katika matabaka matatu ya kawaida: msongamano mdogo, msongamano wa kati na msongamano mkubwa. Watu wa kipato cha chini hukaa katika msongamano mkubwa, na makazi ni madogo sana ikilinganishwa na yale ya msongamano mdogo. Vile vile inatumika katika ulimwengu wa kiroho. Sisi sote hatuko katika ulimwengu au tabaka moja. Hiyo ndiyo sababu kuu ya baadhi ya miujiza na matukio ambayo tunaweza kuwa nayo katika GoodNews World yanaweza kusikika kuwa ya ajabu mahali pengine.

Mtumishi wa Elisha alikuwa katika eneo tofauti na mtu wake wa Mungu. Ambapo alikuwa akiona kifo kinachokaribia, mtu wa Mungu alikuwa akiona ulinzi wa Mungu na uzima. Unaposoma neno hili na kujitoa kwenye maombi, unabadilisha makazi katika roho. Nuru inayoingia kwenye roho yako inakuhamisha sasa hivi. Unasonga kutoka utukufu hadi utukufu, kutoka ukawaida mpaka kwenye maziwa na asali kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nina nuru ya Mungu ndani yangu. Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Nitafaulu katika kila jambo kwa nguvu za Roho Mtakatifu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 12:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 16-18



**Yohana 1:12**
**Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;**

Kuna dhana potofu miongoni mwa jumuiya ya Kikristo ambapo wengi wanaamini kwamba Wakristo ni waamini. Hata hivyo, kulingana na maandiko, sisi si waamini bali ni mazao ya kuamini. Kwa wale wanaoamini, Mungu aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu. Kuamini ni hatua ya msingi au sharti la kuwa mwana wa Mungu. Tumepita kiwango cha kuamini; sisi sasa ni wana wa Mungu.

Wana, watoto wa Mungu waliokomaa, wanajua haki zao na marupurupu waliyo nayo. Wewe si mwamini tena bali ni mtoto mkomavu wa Mungu ambaye ana mapendeleo yote katika Yesu Kristo. Ustawi, afya ya Ki-Mungu na mafanikio yote ni yako. Una uwezo usioshindika wa kuleta mabadiliko katika kila eneo la maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtoto wa Mungu aliyekomaa, na mambo yote mema ni yangu na familia yangu. Nitaishi kutawala leo na siku zote zinazokuja kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:15-17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 19-21



**2 Wakorintho 5:20**
**Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.**

Kuna chumi za dunia ambazo zinachukuliwa kuwa zenye nguvu kubwa katika masuala ya uwezo wa kifedha na nguvu za kijeshi. Nchi nyingi zitajaribu kwa kila njia kutia saini mikataba na kuendana na zile zinazochukuliwa kuwa chumi kubwa ili wapate msaada au ulinzi wakati wa mahitaji. Biblia inatuita mabalozi wa Kristo, ambayo ina maana kwamba hatutoshelezwi kutoka kwenye ulimwengu huu bali kutoka kwa uchumi wa juu, ambao ni uchumi wa Sayuni. Wakati wengine wanashuka, tutakuwa tunasema kuna kuinua.

Sisi ni raia wa Mlima Sayuni, sio wa ulimwengu huu, na katika Mlima Sayuni, hakuna ukosefu au uhitaji. Hutapungukiwa na kitu chochote chema katika maisha haya na yale yajayo. Baba yako, Mungu, ana makundi juu ya milima elfu. Ataendelea kukupa mahitaji yako yote kulingana na utajiri wake katika utukufu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni raia wa Sayuni; mgao wangu ni kutoka juu. Mimi niko vile Mungu asemavyo mimi niko, na ninaweza kufanya kile anachosema naweza kufanya. Nina alama ya mafanikio na mafanikio mwaka huu na daima.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 22-24



**Zaburi 119:130**
**Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga.**

Ninawasikia baadhi ya Wakristo wakiimba "nuru yangu hii ndogo," kana kwamba nuru ya Mungu ndani yako ni kitu ambacho shetani au mazingira yanaweza kupeperusha tu. Hakuna kitu kidogo kuhusu nuru ya Mungu ndani yako. Biblia inasema kufafanusha kwa Neno la Mungu huleta nuru. Je! Unajua tafsiri ya Kigiriki ya neno 'nuru' katika mstari hapo juu ni PHOTIZO, ambayo ina maana ya taa za uwanjani. Unajua mng'ao wa taa za uwanjani; unaweza hata kumuona chungu anayetembea katikati ya usiku. Ni nuru ing'aayo inayofichua hata jambo dogo sana ambalo unaweza kufikiria.

Kupitia Neno hili la Mungu, una aina hiyo ya nuru ndani yako, na hakuna giza linaloweza kustahimili aina hiyo ya nuru ndani yako. Una taa za uwanjani! Toka nje na uangazie biashara yako, familia, afya, elimu, na yote yanayohusu maisha yako!

## UKIRI WA KINABII

**Nina nuru ya Mungu ndani yangu, na ninang'aa. Hakuna kitakachoficha au kuzuia maendeleo yangu kwa jina kuu la Yesu! Utukufu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 5:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 25-26



**Mathayo 5:14**
**Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.**

Ulimwengu umetawala mfumo wa kukutoa ili uwe wa kawaida. Inatamanisha kukufanya usiwe wa kipekee. Unaweza kuwa umefanya shahada fulani katika chuo kikuu katika darasa la wahitimu zaidi ya elfu mbili. Takwimu hii inaashiria kuwa kadiri unavyokuwa na digrii, kuna mtu mwingine mwenye digrii sawa. Uko sawa na kwa kiwango sawa na mtu anayefuata. Kwa hivyo ni nini kitakufanya kuwa wa kipekee? Jibu ni Yesu, ndugu na dada.

Jikabidhi na uyaweke wakfu maisha yako, na Yesu mwenyewe ataleta nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuificha. Wewe ni nuru ya ulimwengu. Hata kama kuna giza, ushindani, na ukosoaji, bado utang'aa kwa Jina la Yesu. Kumbuka huu ni mwaka wa maziwa na asali! Unabii huu na uwe mtazamo wako wa kukufanya mtu asiye wa kawaida

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni nuru ya ulimwengu, na nitaendelea kuangaza. Hakuna kitu kibaya kitakachoweza kunificha kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 27-29



**Kutoka 9:26**
**Katika nchi ya Gosheni tu, walikokaa wana wa Israeli, haikuwako mvua ya mawe.**

Wana wa Israeli walipokuwa Misri, walikaa katika eneo lao lililoitwa nchi ya Gosheni. Lilikuwa ni eneo lililotengwa na Mungu Mwenyewe kiasi kwamba kulipokuwa na giza huko Misri, kulikuwa na mwanga katika Gosheni pekee. Gosheni iliondolewa katika maafa yote ambayo Wamisri walikabili. Mungu alihakikisha kwamba watoto wake mwenyewe hawatapata magonjwa na mapigo ya Misri.

Ni asili ya Mungu kuwalinda na kuwapa mahitaji walio Wake. Mifumo ya ulimwengu huu haitakushikilia kwa sababu, kwa Mungu, uko katika Gosheni yako. Wakati ulimwengu unazungumza juu ya mdororo wa uchumi, kataa kushiriki. Una mgao wako kutoka juu. Nyumba yako ni Gosheni mpya, na utaendelea kuuona mkono wenye nguvu wa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji. Sitakuja kukauka kwa sababu neema ya Mungu yanitosha mimi na familia yangu. Maziwa na asali ni fungu langu langu sifa kwa Mungu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
**Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 30-31**



**Waefeso 5:30**
**Kwa kuwa sisi tu viungo vya mwili wake.**

Maandiko yetu ya leo yanasema sisi ni "viungo vya mwili Wake," ambayo ina maana kwamba sisi ni viungo vya Yesu Kristo. Unapomwona Mkristo, unaona sehemu ya mwili wa Yesu Kristo. Ndio maana tunahitajiana kutengeneza "Mwili wa Kristo."

Ndio maana pia Sauli alipolitesa Kanisa, Mungu aliliona kama shambulio dhidi yake Mwenyewe. Ilichukuliwa kama mateso dhidi ya Mungu Mwenyewe, si dhidi ya washirika binafsi wa Kanisa.

Kila Mungu anapotaka kujongea katika ulimwengu huu wa kidunia, anakutumia wewe. Anatembea na kuzungumza kupitia wewe. Chochote utakachogusa, sio wewe unayekigusa bali ni Mungu. Ukinyimwa mradi, kazi, au visa, si wewe bali Mungu amekataliwa, na Mungu hawezi kukataliwa. Anamiliki kila kitu, wala hana mipaka. Tumia mamlaka juu ya mambo yote ya ulimwengu huu, kwa kuwa wewe ni kiumbe bora zaidi.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiungo cha mwili wa Yesu Kristo. Yesu anatembea hapa duniani kupitia mimi. Nitakuwa mshindi kwa sababu mimi ni mfano wa nguvu katika jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 2:5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 32-34



**Marko 16:15**
**Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.**

Kabla mfalme hajafika, anatuma msafara wake, ambao ni watu wa itifaki yake mwenyewe au timu ya mapema. Msafara unaonyesha ujio wa mfalme kabla hata hajafika. Mungu alinikabidhi mimi na wewe kwenda kuhubiri Injili kwa kila kiumbe kabla ya Mfalme kuja kwa sababu sisi ni wasaidizi wake mwenyewe. Tunatangaza ujio wa Mfalme wa wafalme kwa viumbe vyote.

Kumbuka, kwenye msafara wana silaha, wana ujuzi na wamefunzwa kulibeba jukumu hilo. Mungu pia anakuandaa kwa Neno Lake na mgao wake kwa ajili yako ili utekeleze kazi hiyo. Unaweza usiwe kwenye mimbari kuhubiri, lakini chochote unachofanya, utatimiza kazi hii maalum. Umetiwa mafuta na kutayarishwa ili kutangulia kuja kwa Mfalme wa wafalme. Wewe ni MSAFARA wa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni msafara wa Mungu . Upako wa Mungu u juu yangu kuhubiri Habari Njema kwa viumbe vyote kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 35-37



**Matendo 19:15**
**Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua, na Paulo namfahamu; lakini ninyi ni nani?**

Unapowazia ulimwengu wa roho, unaona nini? Ulimwengu wa kiroho ni ulimwengu, sio tu hewa fulani, kama wengine wanavyoweza kufikiria. Ni eneo na ukanda ambao kuna maisha, vitu vinavyoshikika na uzoefu halisi. Ni halisi zaidi kuliko ulimwengu huu wa kimwili. Unaposhikilia na udhibiti wa ulimwengu wa roho, unaweza kudhibiti kila kitu katika hali ya mwili, kwa maana ni ya kiroho ambayo yanatawala ya mwilini. Kwa maneno mengine, mwili ni zao la roho.

Mapepo waliwajua Yesu na Paulo. Wana wa Skewa hawakuwa maarufu kabisa na hawakuwa na maana katika roho kiasi kwamba hata mapepo hawakuweza kuwatambua. Walikuwa tu watu wasio kitu wakitembea juu ya uso wa dunia. Baba yao alikuwa kiongozi wa kanisa, lakini bado haikuwapa thamani kiroho. Haihusu miunganiko yako lakini haswa ni kuhusu wewe. Leo, chagua kuwa maarufu katika roho kwa Neno la Mungu na maombi.

## UKIRI WA KINABII

**Neno limefurika maishani mwangu. Mimi ni jitu rohoni. Maisha yangu ni maisha ya ushindi na mafanikio katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Marko 16:18**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 38-40



**Mwanzo 1:3**
**Mungu akasema, iwe nuru, ikawa nuru.**

Sonolumineisensi ni jambo katika fizikia ambalo linathibitisha kisayansi kwamba sauti hutoa nishati ambayo hutoa mwanga. Hii ni teknolojia iliyoundwa na Mungu ili kwamba wakati Alipozungumza, alitoa mawimbi ya sauti, na mawimbi hayo ya sauti yakaumba mwanga. Alipokuumba kwa mfano wake, alikupa uwezo huo huo ili nawe utoe nuru unapozungumza. Elewa kwamba unapozungumza, hutoa sauti kutoka katika kile kilicho ndani yako na kisha kuielekezea kwa nje. Ndivyo ilivyo katika ulimwengu wa kiroho.

Biblia inasema, "Kufafanushwa kwa maneno yako kwatia nuru [huonyesha au huwa]!" Kwa hivyo, ili uweze kutoa nuru kwa nje, nuru lazima kwanza ikuingie. Maandiko yanatuambia kwamba kuingia kwa Neno la Mungu ndiko kunaleta nuru hiyo ndani yako. Kwa maneno mengine, katika ulimwengu wa Roho, maneno hupimwa kwa nuru. Tunazungumza kwa kutoa nuru. Kwa hivyo, kiasi cha nuru ulicho nacho ni kiasi cha msamiati unaoweza kunena katika Roho kwa nuru. Jenga msamiati wako kila siku kwa kuzama katika Neno la Mungu. Unapotamka ujue kuwa kila kitu kuhusu maisha yako kinabadilika kuwa maziwa na asali!

## UKIRI WA KINABII

**Nuru yangu inaongezeka, na kwa uwezo wa Neno ndani yangu, ninaachilia nuru katika afya yangu, fedha, familia, na kubadilisha kila hali mbaya inayonizunguka kuwa faida yangu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 119:130**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 41-42



**2 Wakorintho 5:14**
**Maana upendo wa Kristo watubidisha maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote;**

Kuna jambo fulani kuhusu mtazamo wa kahaba ambalo kila Mkristo anapaswa kuiga. Hiyo inaweza kuonekana kama wazimu, lakini nitaelezea. Umewahi kuona jinsi kahaba anavyohakikisha bidhaa yake inawekwa bayana kila wakati ili kila mteja anayetarajiwa ajue anachouza? Analazimika kufanya hivyo kwa sababu anatambua thamani ya bidhaa yake, na anaelewa kuwa yeye ndiye mtu bora zaidi wa kuitangaza. Anazungumza akiwa na lengo moja akilini, nalo ni kutangaza bidhaa yake. Licha ya hali ya hewa, mvua au radi, atakuwa huko nje akiuza. Zaidi ya hayo, ikiwa kona aliyopo haivutii wateja anaowataka, atatafuta kona nyingine.

Elewa kwamba bidhaa kuu ya Mungu ni Yesu, na kila Mkristo ni muuzaji mteule Wake. Kwa hivyo, kama Mkristo, usifiche Bidhaa ya Mungu kamwe. Unapozunguka, acha Biblia yako ionekane. Usiifiche. Badala yake, onyesha kwa ufahali kabisa. Unapozungumza, acha mazungumzo yako yawe chombo cha uuzaji kinachoelekeza wengine kwa Yesu. Kubali mtazamo kwamba iwe mvua au jua, katika yote ufanyayo, utamkuza Yesu hata iweje!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni tangazo hai, linalotembea, linalozungumza la Bidhaa kuu zaidi ulimwenguni! Mimi ndiye muuzaji nambari moja wa Bidhaa inayoitwa Yesu, na sitachoka kamwe, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**2 Wakorintho 3:2**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 43-45



**Mithali 3:9**
**Mheshimu BWANA kwa mali yako Na kwa malimbuko ya mazao yako yote (mapato).**

Usimamizi wa mali unarejelea usimamizi wa kimkakati wa rasilimali za kifedha za mtu binafsi ili kusaidia kufikia malengo yao ya kifedha. Ulimwengu una njia zake za kuendesha mfumo huu, lakini sisi si wa ulimwengu huu. Mungu ametupa mfumo wetu wa kupata, kuongeza na kulinda fedha zetu, hata kabla hazijafika. Mfumo wa kifedha wa ulimwengu unahusisha kuweka akiba, lakini katika mfumo wa Mungu, njia ya kupata udhibiti wa kifedha usio na shaka ni kwa kutoa.

Zaka ni chombo katika mfumo wa fedha wa Mungu unaokupa uwezo wa kufanikiwa. Ndani ya mfumo huu, una uwezo wa kudhibiti na kuharakisha faida yako kwa kuwekeza au kutoa, si kulingana na salio la benki yako au bajeti inavyoelekeza, lakini kulingana na kile unachotarajia kama faida. Umepewa uwezo wa kutoa zaka kulingana na kile unachotarajia kupokea. Amua unachotaka kipato chako kiwe, kisha weka lengo lako kuanza kutoa zaka kwa kiwango hicho au kuelekea kiwango hicho sasa. Usiruhusu kamwe salio lako la benki kuamua uwezo wako wa kutoa. Badala yake, toa kulingana na mavuno unayotarajia, na utaona maajabu katika fedha zako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninasukuma fedha zangu katika ulimwengu wa roho ambapo mharibu hawezi kuzigusa. Nimepakwa mafuta kusimamia mali. Fedha zangu zinalindwa, na pesa zinakuja kwangu kama maziwa na asali kwa Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Mithali 3:9-10**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 46-47



**Ufunuo 1:16**
**Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume, na upanga mkali wenye makali kuwili ulitoka katika kinywa chake;**

Kuna kiwango fulani cha kinga ya kidiplomasia, usalama wa mbinguni ambao baadhi ya Wakristo wametambua, kwamba wanaweza kusema lolote wakati wowote, na likatokea. Pendeleo hili si kwa watu wachache waliochaguliwa katika Jumuiya ya Wakristo. Pia una uwezo wa kufanya hivyo kupitia maombi. Siri ya Ukristo iko kinywani mwako. Kinywa chako si kwa ajili kula. Kwa hakika, tafsiri ya Kigiriki ya 'mdomo' ni stoma, ambayo ina maana ya kisu unachotumia kukata kitu katika vipande vipande. Unapoelewa hili, utagundua jinsi maombi yako yalivyo hatari.

Maombi ni kombora la kuvuka mabara ambalo unaweza kulitumia kuharibu umaskini, magonjwa, na aina yoyote ya kushindwa. Shirikisha akili yako unapoomba ili uwe na ufahamu wa silaha unayotumia. Unapoomba kwa Baba katika Jina la Yesu, anza kujiona wewe mwenyewe ukiuchoma ugonjwa huo, kushindwa huko, talaka hiyo, umaskini huo kwa kudunga kwa kisu! Tumia stoma yako - mdomo wako - kukata na kukata kila kitu ambacho kinajaribu kuzuia maendeleo yako!

## UKIRI WA KINABII

**Mungu anasema mimi ni tajiri; kwa hivyo, sitakufa mpaka nimiliki maziwa na asali yangu! Hakuna ugonjwa utakaoniondoa katika ustawi wangu. Hakuna kitakachokatiza amani ya moyo wangu, ndoa, au uhusiano wowote uliopangwa na Mungu, katika Jina Kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Timotheo 1:18**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mwanzo 48-50



**2 Wakorintho 6:14**
**Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?**

Maisha ya Kikristo ni juu ya kuondoa data ya kishetani na kuibadilisha na data takatifu ya kiroho. Kwa kweli, kiasi cha mwanga ndani yako kinaweza kupimwa kwa kiasi gani cha giza ambacho umeondoa kutoka karibu nawe. Ndiyo maana katika Yohana 14:30, Aliweza kutangaza kwa ujasiri kwamba shetani "hana kitu kwangu. [Hana uhusiano wowote na Mimi; hakuna chochote ndani Yangu ambacho ni chake, na hana uwezo juu Yangu.] " Aliwezaje kutoa madai hayo ya ujasiri? Ni kwa sababu Alijua ustadi wa kuondoa data za kishetani.

Hii ndio sababu unapaswa kuwa mwangalifu ni nani unayefanya nae urafiki. Huu ndio ushauri ambao Biblia imetoa. Watu wengine huingia katika maisha yako ili tu kufuatilia na kuzuia maendeleo yako. Hutoa mwanga hasi unaovutia shughuli za kishetani. Fanya uamuzi wa kuishi maisha yaliyopangiliwa. Jiambie sitafanya lolote isipokuwa Mungu yumo ndani yake, isipokuwa kama linalitukuza jina la Mungu, na ni kwa ajili ya huduma yangu binafsi kwa ajili ya Mungu. Chagua kujiondoa kwa mtu yeyote anayeshirikiana na giza ambalo umeamua kuliondoa kwenye maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kuishi maisha yaliyopangiliwa, yasiyo na ushawishi wa giza. Ninaamuru na kutangaza, kila data ya kipepo imeondolewa kutoka kwenye maisha yangu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Wakorintho 15:33**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 1-3



**Waebrania 11:3**
**Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.**

Zisizoonekana kwa macho yetu ni molekuli za hidrojeni na oksijeni, lakini kupitia muunganiko wa kemikali huwa dutu inayoonekana inayoitwa maji. Mungu alianzisha michakato hii isiyoonekana katika uumbaji ili kuitikia kwa muendelezo kwa Neno Lake ili kufanyiza vitu vinavyoonekana vinavyoleta maana kwenye maisha yetu.

Amefanya vivyo hivyo katika ulimwengu wa roho. Jeni zetu za kiroho zinabeba uwezo wa ubunifu wa kuumba ulimwengu wetu binafsi kwa mawazo na maneno tunayofikiri na kuzungumza, ambayo ni zana za ki-Mungu zinazotolewa kwa matumizi yetu ya ubunifu.

Tumezingirwa na "molekuli" za kiroho ambazo zimeundwa kuitikia mawazo na maneno yetu, au zaidi tukiliweka kimaandiko, imani yetu ya kuzalisha miujiza. Kwa kuwa ulimwengu wa roho ndio ulimwengu wa kawaida, basi muujiza wako daima uko kwenye mwendo. Ninaposema, pesa zinakuja, ile tu kwamba ninazungumza, inamaanisha, utaratibu wa kuzileta pesa kwako tayari umewekwa, ni zako kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nina nguvu ya uumbaji kinywani mwangu. Ninachochea msukumo wa kuumba muujiza wangu ninapotamka. Nina asili ya Uungu ya Mungu na najua ninatembea katika mamlaka ya Ki-Ungu katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 33:6**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 4-6



**Luka 10:19**
**Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.**

Mstari hapo juu unasema kwamba Mungu aliwapa watoto wake mamlaka juu ya nguvu zote za adui, si baadhi, si nyingi sana, lakini ZOTE! Hii ina maana kama Wakristo, una uwezo wa kutangaza uzima katika hali yoyote iliyokufa, iwe ni umaskini uliolemaa au ugonjwa - umepewa uwezo wa kushinda. Kama mtoto wa Mungu, ni muhimu kwamba utumie mamlaka hiyo ambayo ulipewa bure pale ulipomkubali Kristo maishani mwako.

Katika Biblia, kuna matukio kadhaa ambayo tunaweza kutaja ambayo yanaonyesha mashujaa wa imani yetu kuwa na ufahamu wa mamlaka yao ya kiroho. Hili linaonyeshwa pale Mtume Paulo anaposema katika 2 Wakorintho 10:4, 'Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu." Licha ya mateso makali ambayo Paulo alikumbana nayo wakati wote wa uandishi wa kitabu hiki mahususi cha Biblia, alidumisha ufahamu wa mamlaka yake katika Mungu! Bila kujali misukosuko ya maisha unayokabiliana nayo, chagua kutembea katika ufahamu ambao Mungu amekupa nguvu juu ya shetani!

## UKIRI WA KINABII

**Leo nachagua kutambua Mamlaka yangu ya Kiroho katika Kristo. Nimepewa uwezo wa kushinda hali yoyote ninayoweza kukabiliana nayo. Ushindi wangu umeshapangwa katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Yohana 4:4**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 7-9



**Yakobo 2:26**
**Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.**

Wajibu wetu kama Wakristo ni kulifanyia kazi Neno! Wakristo wengi wanajivunia kuhudhuria ibada na ratiba za kanisa mara kwa mara, lakini maisha yao yanabaki vile vile! Ingawa wengine wanaweza kupendekeza kwamba mhubiri ana makosa, ni kinyume chake! Watu wengine hufanya makosa kwa kusikia tu Neno bila kulifanyia kazi. Biblia iko wazi juu ya sifa mbaya za kuwa msikiaji wa Neno pale tu linaposema katika Yakobo 1:22, 'Iweni watendaji wa neno, si wasikiaji tu hali mkijidanganya nafsi zenu.' Hii inatuambia kwamba wale wanaosikia wanaishi maisha ya ukengeufu tu!

Jifunze kutumia Neno la Mungu katika kila eneo la maisha yako. Neno letu la rhema kwa mwaka huu ni maziwa na asali, kwa hiyo kataa kuwa kama wale wanaosikia neno hili lakini hawalitendi. Biblia inasema Neno ni chombo cha kutuandaa kwa kila kazi njema. Mara tu unapoanza kulitenda Neno la Mungu, utapata ukuaji mkuu katika nyanja zote za maisha yako na kurandwa kikamilifu kwa ajili ya KILA kazi njema!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni Mkristo mtoa uthibitisho, si msikiaji tu wa Neno bali pia mtendaji. Ninaposikia Neno, ninatayarishwa kwa kila kazi njema. Katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Petro 1:13**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 10-12



**Mathayo 6:27**
**Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja?**

Katika ulimwengu unaokaribia mwisho wake, unaotutia hofu kila mara kwenye taarifa na aina zote za vyombo vya habari vya kawaida, ni rahisi kukengeushwa na sauti za nje. Pamoja na hayo, mstari unasema wasiwasi hauongezi chochote katika maisha yako! Kama Mkristo, jiambie kuwa wasiwasi ni jambo lisilo na msingi wowote.

Biblia inasema kwamba Mungu huwajalia hata ndege wa angani; si zaidi WEWE, Mtoto Wake! Kataa kuruhusu hofu itawale maisha yako. Neno linasema acha kesho ijisumbukie yenyewe. Hii ina maana kila siku imepewa jukumu la kujisumbukia, sio wewe! Tunajua kama wana wa Mungu, tumeondoa mzigo wa wasiwasi katika maisha yetu, na wale waliochoka na kulemewa wamepewa pumziko ndani ya Baba!

Mungu humpa kila mmoja wa watoto wake amani isiyo na kifani. Wasi wasi kwetu unapaswa kuwa dhana ya ajabu ambayo haiwezekani kueleweka! Kataa wasi wasi kila wakati, iwe katika biashara, kazini au maisha yako ya familia. Kataa kuwa na wasi wasi na kuruhusu maisha yako yaakisi wema wa Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha ya utele! Pesa zitakanyagana kupitia milango ya biashara zangu! Sina hofu kwa CHOCHOTE. Ninaishi maisha YASIYO NA WASI WASI, ya namna ya MAZIWA na ASALI katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Petro 5:7**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 13-15



**Zaburi 16:11**
**Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako ziko furaha tele; na katika mkono wako wa kuume kuna mema ya milele.**

Shangwe inategemea matukio, ambapo furaha ni uamuzi ambao kila mtoto wa Mungu anapaswa kufanya. Ona nimesema ' uamuzi ', si ' hisia '. Biblia inatuambia tuhesabu kuwa ni furaha tupu tunapoangukia katika majaribu mbalimbali. Hii ina maana furaha haitegemei hali bali uamuzi.

Mstari maarufu miongoni mwa wahubiri na makutaniko mengi unasema, ' Furahini katika Bwana siku zote ' (Wafilipi 4:4). Wakristo wengi hawatambui mazingira ambayo kifungu hiki kiliandikwa. Paulo alikuwa anaandikia kanisa la Filipi akiwa gerezani! Hata hivyo, licha ya hali zenye kuogofya alizokuwa nazo, Paulo aliweza kubaki mwenye furaha katika hali hiyo yote.

Mungu amewapa watoto wake wote silaha ya furaha. Biblia inasema furaha ni dawa nzuri, bali roho iliyopondeka huikausha mifupa. Hii inatuonyesha kwamba kutochagua kuwa na furaha kuna madhara katika maisha yako. Leo, chagua kumchanganya adui kwa kuwa na furaha bila kujali hali yako!

## UKIRI WA KINABII

**FURAHA NI SILAHA YANGU, na kiwango changu cha furaha kinawachanganya maadui zangu. Ninachagua kuwa na furaha bila kujali kinachotokea kunizunguka leo katika Jina Kuu la Yesu! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Yohana 16:24**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 16-18



**Waebrania 6:10**
**Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata mngali sasa hivi.**

Iwe unasaidia kupanga viti kabla ya ibada au ni kiongozi wa kuabudu au mhubiri katika kanisa lako, Mungu hasahau kamwe kazi yako ya upendo! Kazi yako ya kupeleka mbele Ufalme wa Mungu kamwe haiendi bila kutambuliwa na Bwana Yesu na inathawabishwa sana.

Je, hiyo haishangazi jinsi ambavyo Mungu hasahau kamwe yote ambayo umefanya kwa ajili ya Ufalme? Biblia inatuambia kwamba wale wanaotafuta kwanza Ufalme na haki yake, vitu vyote vitazidishwa kwao. Ingawa wokovu ni zawadi inayotolewa bure na si kwa matendo yetu, Yesu ana thawabu maalum zinazowangoja wale waliojitoa na kuendeleza Ufalme Wake.

Wale wanaofadhili uenezaji wa Injili pia wanathawabishwa. Biblia inatuambia kwamba wanaotoa kwa siri, Mungu atawalipa hadharani! Unapoendelea kutembea katika wito wako, fahamu kwamba kujitoa kwako na uaminifu wako kwa mambo ya Mungu hakupotei bila kutambuliwa, na utatuzwa maziwa na asali kulingana na kazi zako!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni askari katika Ufalme wa Mungu. Mungu ana thawabu maalum kwa kujitoa kwangu kwenye Injili. Kujitoa kwangu hakupotei bila kutambuliwa, na nitalipwa hadharani kwa yote ambayo nimefanya faraghani, katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Wakorintho 3:13-14**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 19-21



**Waebrania 13:2**
**Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.**

Katika baadhi ya mwingiliano wetu wa kila siku, tunaweza kuwa tunaburudisha malaika bila kujua. Kwa hivyo, kama watoto wa Mungu, ni muhimu sana kwamba kuna tofauti kubwa kati ya tabia yako na ile ya wale wanaoishi ulimwenguni. Biblia inasema katika 1 Petro 1:15, ‘ Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.’ Maandiko haya yanatuonyesha tunatarajiwa kuenenda kwenye njia ya Ki-Mungu katika namna YOTE ya mazungumzo. Unapoendelea na siku yako, iwe shuleni, chuo kikuu au kazini kwako, enenda katika njia ya Kiungu; hujui kila mara unashirikiana na nani!

Popote tunapoenda, lazima tuwe kielelezo, si kwa wasio Wakristo tu bali pia kwa Wakristo katika maneno, mazungumzo, mapendo, roho, imani na usafi. Usiruhusu kamwe hisia zako na hali zinazokuzunguka kubadilisha jinsi unavyojiweka; katika kila ufanyalo, uwe mfano kwa wenzako na mwanga katika jamii yako!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtoto wa Mungu; Ninaenenda katika njia ya Ki-Mungu popote niendapo. Ninaishi maisha ya kujitenga mbali zaidi ya mifumo ya ulimwengu huu. Mwaka huu, nitakuwa mfano kwa wenzangu, katika Jina Kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Yohana 2:6**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 22-24



**Waebrania 2:8**
**Umeviweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake, hakusaza kitu kisichwekwa chini yake. Lakini sasa bado hamjaona vitu vyote kutiwa chini yake.**

Kihalali, Mungu ameweka vitu vyote chini ya mamlaka ya wanadamu, lakini katika uzoefu wa kibinadamu, hatuoni! Wakristo bado wametawaliwa na magonjwa na umaskini, lakini hili si kusudi la Mungu kwa maisha yetu! Kuna uwezekano usio na kipimo kwa mtoto wa Mungu; una uwezo na mamlaka ya kuharibu kila ukuta ulio mbele yako. Jitangazie mwenyewe kila siku kuwa fedha zako, afya yako, VITU VYOTE viko chini ya miguu yako! Biblia inasema Mungu ametupa vitu vyote vinavyohusu uzima na utauwa. Ukigundua hili mapema, ndivyo utakavyoona mabadiliko katika maisha yako ya kila siku.

Kulikuwa na watu katika Biblia ambao walikataa kushindwa na hali zao. Musa alikuwa kati ya Wamisri na Bahari ya Shamu; alipaniki? HAPANA! Alikataa kuona kuta mbele yake na kugawanya maji! Kataa kutambua ukuta wowote unaojaribu kukuzuia!

## UKIRI WA KINABII

**Vitu vyote viko chini ya udhibiti wangu. Mimi ni mpira wa kubomoa unaogonga ukuta wowote uliopangwa ili kunizuia! Maisha yangu ni matamu kama asali, katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 82:6-7**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 25-27



## MUNGU WA UWEZEKANO USIO NA UKOMO

Kuna uwezekano usio wa kikomo kwa wale wanaomwamini Mungu. Biblia inatuambia katika andiko hilo hapo juu kwamba mambo yote yanawezekana kwa Mungu! Hii ina maana hakuna hali Mungu hawezi kutatua, hakuna ukame ambao yeye si dawa. Kama Wakristo, tumepewa uwezo wa kupambana na hila na hila zote za shetani; hakuna lililo gumu kwa Bwana!

Katika Biblia tunaona miujiza, ishara na maajabu yasiyoweza kufikirika, kuanzia watu kufufuliwa kutoka kwa wafu, magonjwa yakiondolewa kutoka kwenye miili ya watu, na bahari nzima kugawanywa vipande viwili. Hata hivyo, Yesu alisema tutafanya kazi kubwa zaidi! Hii ina maana kwamba kama mtoto wa Mungu, una uwezo wa kukiri uponyaji katika mwili wako mwenyewe na fedha katika maisha yako! Yesu aliweka nguvu ndani yako kufanya lolote kabisa!

Biblia inatuambia kwamba Kristo hututia nguvu kufanya mambo YOTE; Nguvu za Mungu zinatosha kufidia udhaifu wetu! Unapoendelea na mtembeo wako na Kristo, fahamu kwamba hakuna vikwazo kwa kile unachotaka kutimiza katika mwaka huu wa maziwa na asali ikiwa tuu unaamini!

## UKIRI WA KINABII

**Kwa njia ya Kristo naimarishwa kufanya mambo YOTE. Katika mwaka huu, hakutakuwa na KIKOMO kwa kile ninachopata! Afya yangu ni nzuri! Nitazidi matarajio ya wenzangu, na kiasi kisichoelezeka cha mali kitanijia haraka kuliko duma katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Wafilipi 4:13**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 28-29



**Wagalatia 5:24**
**Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.**

Kama Wakristo, sisi si watumwa wa mwili na tamaa zake! Umetengwa na ulimwengu huu; hii ina maana wakati dunia inakabiliwa na ukame, ukame si sehemu yako. Biblia inasema hatupaswi kufuata mtindo wa ulimwengu huu, ikimaanisha ambapo ulimwengu unakumbwa na tauni na milipuko ya magonjwa, tunapata afya na miujiza isiyo na kifani!

Neno linasema sisi ni MIUNGU! Kila siku fahamu kuwa wewe ni kiumbe cha roho na uko juu ya mifumo na kanuni za ulimwengu huu. Matamanio ya dunia yote ni ubatili! Kataa kukubali sauti zinazosema kinyume na Neno la Mungu na kujaribu kukushawishi kufanya mabaya.

Ukiamua kujisalimisha kwa Mungu na kumpinga shetani, atakukimbia! Biblia inatuambia kwamba kuwaza juu ya mwili ni uadui kwa Mungu. Ndiyo maana tunaambiwa lazima tufanye upya nia zetu! Hakikisha kama Mkristo kwamba akili yako imeimarishwa na Neno la Mungu. Usiruhusu sauti yoyote ya nje kukushawishi au kukupotosha! Unafikiri tofauti na wale walio duniani. Wewe hauko katika MWILI!

## UKIRI WA KINABII

**Sipo katika mwili! Nimeusulubisha mwili na tamaa zake zote, katika Jina la Yesu Mwenye Nguvu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Warumi 6:23**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Zaburi 30-32



**Mathayo 10:31**
**Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi.**

Kwa Mungu, baadhi ya watu ni wa KUJITOA MUHANGA! Ingawa hiyo inaweza kuja kama mshtuko, kaa nami. Kila Mkristo anaweza kuongeza thamani yake ndani ya Ufalme wa Mungu na kuwa asiye na mbadala machoni pa Mungu. Katika Biblia, shetani alidai mtumishi wa Mungu Ayubu (mtu mwenye mali nyingi na mwadilifu) angemkana ikiwa angenyang'anywa vyote alivyokuwa navyo. Mungu alimruhusu Shetani amjaribu Ayubu lakini hakumruhusu asimdhuru mtoto Wake kimwili kwa njia yoyote ile. Ingawa Mungu alimkataza shetani asimdhuru Ayubu, shetani aliruhusiwa kusababisha wavamizi kuvamia na kuwaua wakulima wa Ayubu.

Hilo linaonyesha kwamba Mungu ana wale walio wa muhimu zaidi kuliko wengine ndani ya Ufalme. Biblia inatuambia kwamba unapokuwa wa muhimu kwa Mungu, unakuwa kipaumbele chake kikuu, naye atatoa taifa zima ili tu kukuokoa!

Ukiwa mtoto wa Mungu, unaweza kuongeza thamani yako katika Ufalme kwa kushiriki tu katika kazi ya huduma. Kushiriki katika programu na shughuli mbalimbali za kanisa zinazohusu kuendeleza Ufalme wa Mungu kunaweza kuongeza umuhimu wako. Iwe unaimba, kufanya usafi, au hata kucheza, ruhusu kipawa chako kiwe baraka kwa Ufalme wa Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kuongeza thamani yangu leo! MIMI ni wa MUHIMU kwa MUNGU; Ninaongeza thamani isiyopingika kwa Ufalme, katika Jina Kuu la Yesu ! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Isaya 43:4**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 33-35



**Zaburi 41:3**
**BWANA atamtegemeza alipo mgonjwa kitandani; katika ugonjwa wake umemtandikia.**

Mstari ulio hapo juu unaeleza jinsi Mungu anavyoweza kuwarudisha wale walio kwenye vitanda vyao wagonjwa katika afya kamilifu! Biblia inatuambia kwamba kwa kupigwa kwa Yesu, tuliponywa. Kama Mkristo, ni muhimu kwamba uzungumze na ugonjwa na kuuamuru uondoke kwenye mwili wako. Kama vile imani huja kwa kusikia na kusikia kwa Neno la Mungu, hofu huja kwa kusikia na kusikia kwa maneno ya shetani.

Kataa kutega masikio yako kwa sauti ya mdanganyifu na umlenge Yesu Kristo pekee. Imani katika kiwango cha msingi ni mabishano na shetani; anapojaribu kusema wewe ni mgonjwa, tamka uponyaji katika kila nyuzi za uhai wako. Katika kila hali, dumisha ungamo lako!

Sio tu kwamba tuna uwezo wa kukiri uponyaji katika miili yetu wenyewe, lakini ya watu wengine pia! Mungu amempa kila mmoja wa watoto wake mamlaka isiyo na shaka juu ya mambo yote yahusuyo maisha na utauwa. Tembea katika ufahamu kwamba ugonjwa hauna nafasi katika maisha yako au ya familia yako. Mara tu unapotambua uwezo wako uliopewa na Mungu, ugonjwa hautakuwa na chaguo ila kuondoka!

## UKIRI WA KINABII

**Ugonjwa hauna nguvu katika maisha yangu! Nina uwezo wa kuondoa ugonjwa kutoka kwenye mwili wangu. Afya yangu ni ya KIVUTIO na inatiririka maziwa na asali, katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Petro 2:4**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 36-38



**1 Wathesalonike 5:17**
**...Ombeni bila kukoma.**

Kama watoto wa Mungu aliye hai, lazima tuombe bila kukoma! Maombi sio kila kitu, lakini yanabadilisha kila kitu! Maombi ni teknolojia ambayo unaweza kuwasiliana na Baba. Kupitia maombi, tunahuishwa na kuchajiwa! Mahali pa maombi ni mahali pa ukarabati na kuatamiwa. Wanaume wa maombi wanahama kutoka kuishi hadi umilele! Watu wa maombi wana thamani isiyopingika katika Ufalme wa Mungu.

Ndiyo maana Biblia inatuambia juu ya sauti ya Abeli iliyomlilia Mungu hata katika kifo. Abeli alikuwa amejijenga sana katika Ufalme kupitia sala yake kiasi kwamba sauti yake ilibaki kusikika kwa Mungu. Hakikisha nyumba yako ni nyumba ya maombi. Maombi yana uwezo wa kubadilisha maisha yako na ya familia yako. Jua kwamba unapounda mazungumzo ya wazi na Mfalme wa Wafalme, maombi yako, bila ubaguzi wowote, yanajibiwa kwa ndiyo na amina kabla hata hujaanza kuomba.

Hii ndiyo sababu kuwa thabiti katika maombi ni muhimu ili kuanzisha uhusiano na Mungu. Katika Biblia, tunaona wanafunzi wa Mungu wakitoa masaa katika siku zao ili kuomba na kumwabudu Mungu; hii ina maana ni muhimu kuheshimu saa zilizotengwa za maombi ndani ya kanisa lako husika. Bila kujali kinachoendelea katika maisha yako, hakikisha unatenga muda kwa ajili ya maombi.

## UKIRI WA KINABII

**Kuna nguvu katika maombi yangu! Maombi yangu yanabadilisha kila ukungu na utangotango wa maisha yangu kuwa maziwa na asali! Katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Wafilipi 4:6**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kutoka 39-40



**Zaburi 133:1**
**Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, ndugu wakae pamoja, kwa umoja!**

Kama Wakristo, lazima tufanye kazi pamoja kwa umoja mkamilifu, usioyumba! Ulimwengu umetawaliwa na ubaguzi, udini, na siasa za utambulisho; hizi ni sifa ambazo huwezi kuruhusu ziingie kwenye mtembeo wako na Mungu. Haijalishi itikadi au asili ya mtu, mheshimu sana kila jirani yako.

Biblia inatuambia kwamba kwa kupendana, tunatambuliwa kuwa wafuasi wa Yesu Kristo. Hakikisha haufanyi chochote kwa tamaa ya ubinafsi au majivuno ya bure lakini badala yake fanya kila kitu kwa unyenyekevu, ukiwathamini wengine kuliko wewe mwenyewe! Wewe ni mlinzi wa ndugu yako! Pale kaka au dada katika Kristo anahitaji msaada, acha silika yako ya kwanza iwe kuwasaidia kwa njia bora uwezavyo. Hizi ndizo sifa tunazotarajiwa kuwa nazo kama watoto wa Mungu.

Kanisa ni utimilifu wa Kristo! Kristo amedhihirishwa kijumla na kikamilifu katika Kanisa lake, ambalo ni mwili wake! Utimilifu wa Kristo unaonyeshwa na kuthibitishwa kupitia mwili wake katika Neno. Kila kitu kinachohusiana na Yesu Kristo kiko katika Kanisa Lake; Utukufu wake na tabia ziko katika Kanisa Lake. Hii ina maana kama mwili ulioungsanishwa, SOTE tumerithi sifa za Kristo!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni MTATUZI wa matatizo! Popote msaada unapohitajika, Mimi ndiye SULUHISHO. Ninawatunza kaka na dada zangu katika Bwana, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Waefeso 4:3**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 1-4



**Waefeso 3:19**
**na kuujua upendo wa Kristo upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika katika utimilifu wote wa Mungu.**

Upendo ni ujumla wa asili ya Mungu; Yeye ni upendo uliofanyika mtu! Matokeo yake, ndani ya Kristo kuna upendo unaopita ufahamu wote wa kibinadamu. Biblia inatuambia kwamba Mungu anakupenda sana kiasi kwamba alimtoa Mwanawe, Yesu Kristo, ili upate uzima wa milele. Ijapokuwa wale walio duniani wanaweza kuamsha hisia zao kwako kulingana na hali mbalimbali au hata hatua ambazo umechukua dhidi yao, upendo wa Mungu unaelezwa kuwa usio na mwisho, kumaanisha kabisa hakuna kitu kinachoweza kukutenganisha na upendo wa Kristo!

Ulipomkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako, Roho Wake alikumiliki mara moja kwa upendo Wake. Kwa hiyo, tukiwa Wakristo, ni muhimu kuwa na upendo kama vile Baba yako anavyopenda. Unapoendelea katika kutembea kwako na Kristo, ukiufanyia kazi upendo wako kwa wale wanaokuzunguka, unakuwa kama Baba yako. Biblia inatuambia kwamba upendo wa Mungu umemiminwa katika mioyo yetu; kwa hivyo, haiwezekani kutopenda kama Mkristo! Ukiwa kama matokeo ya upendo, lazima uonyeshe si kwa maneno yako tu bali pia kwa matendo yako. Katika muda uliosalia wa juma hili, chagua kutembea katika upendo wa Mungu!


## UKIRI WA KINABII

**MUNGU ananipenda sana! Nina asili sawa na Baba, katika Jina Kuu la Yesu .**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Yohana 4:7-8**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 5-7

# WORKING TOGETHER AROUND THE WORLD TO DELIVER THE GOODNEWS OF JESUS CHRIST TO EVERY COUNTRY.



INDIA



RWANDA



GERMANY



FIJI



USA



UK

# GoodNews DAILY



NIGERIA



FRANCE




ZIMBABWE



BELGIUM



JOHANNESBURG



AUSTRALIA

**AS COLD WATERS TO A THIRSTY SOUL, SO IS GOODNEWS FROM A FAR COUNTRY. (PROVERBS 25:25)**

WWW.GOODNEWSWORLD.COM/GOODNEWSDAILY



**Yeremia 29:11**
**Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho**

Mungu ana mipango ya ajabu kwa ajili yako! Jua kwamba kama mtoto wa Mungu, mahitaji yako yote hutolewa kulingana na utajiri wake katika utukufu. Hii ina maana kwamba uhaba hauna nafasi katika maisha yako. Unaweza kuishi maskini, lakini jua kwamba hakuna Mkristo aliyezaliwa ili awe mgonjwa, mwenye huzuni, au maskini. Kusudi la Mungu ni wewe kufanikiwa katika kila jambo unalochagua kujihusisha nalo. Kataa kuuridhia au kuukubali umaskini katika maisha yako au ya familia yako! Kiri kwamba Mungu aliondoa umaskini wako mara tu ulipokuwa Mkristo. Ongea na hali yako ukisema, Sipungukiwi KITU!

Faida za kuwa na mafanikio ziko wazi kabisa! Katika Mwanzo, mafanikio yanaelezewa kama kimbilio na uzio wa ulinzi dhidi ya shetani. Biblia inatuambia kwamba licha ya majaribio ya shetani, hakuweza kumdhuru mtumishi wa Mungu Ayubu kutokana na wigo wa fedha uliomzunguka yeye na nyumba yake. Endelea kukiri mambo chanya tu juu ya maisha yako na fedha. Kadiri unavyotambua utajiri wako katika Kristo, ndivyo uzio wa utajiri utakukimbilia na kukuzunguka!

## UKIRI WA KINABII

**Nina HELA NYINGI SANA! Ninavutia utajiri usio na kikomo, usioweza kutafutwa na kiasi kikubwa cha pesa! Mungu amebariki kazi ya mikono yangu! PESA ZINANIJIA KAMA MAZIWA NA ASALI SASA! Utukufu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Mhubiri 7:12**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 8-10



**Yohana 4:35**
**Hamsemi nivyi, Bado miezi minne ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, Inueni macho yenu, myatazame mashamba; ya kwamba yamekwisha kuwa nyeupe tayari kwa mavuno.**

Kuvuna nafsi ni rahisi! Yesu tayari amejibu kila pingamizi linalowezekana linalokuaminisha kwamba kuvuna nafsi ni kugumu. Shida ni kwamba wakristo wamesoma maandiko juu ya kuvuna nafsi lakini hawajapata muda wa kuzama ndani zaidi kwenye kile ambacho Mungu alisema. Yesu (mkuu wa kuvuna nafsi) alielewa upendo wa Wayahudi kwa kilimo na akautumia kama msingi wa mafundisho haya.

Ili kuelewa swali lililoulizwa katika mstari wa usomaji wa leo , ni lazima uelewe kwamba inachukua muda wa miezi minne kwa ngano kukomaa kabla haijawa tayari kuvunwa na mkulima, na Bwana anatumia lugha hii kwa makusudi, akijua wasikilizaji wake.

Sasa, wewe si mkulima! Kwa hivyo, sio jukumu lako kukuza misingi ya kuvuna roho. Ilikuwa tayari imefanywa na Mungu! Hii inabatilisha kabisa imani kwamba kuvuna nafsi ni kugumu. Wanaofikiri namna hii wamekosea kwa kujipa nafasi ya mkulima wakati jukumu hilo ni la Mungu pekee! Kuwa mvuna nafsi mkuu ni kutambua uhusika kwa Mungu kama mkulima! Mavuno yako tayari kwako ili kuvuna nfsi LEO!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni MVUNA NAFSI MKUU! Kuvuna nafsi kumerahisishwa kwangu. Mavuno YAKO TAYARI! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Mithali 11:30**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 11-13



**Mithali 18:21**
**Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi, nao waupendao watakula matunda yake.**

Maneno yako yana nguvu! Kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, Mungu hajafanya chochote kimwili; yote aliyofanya ni kusema! Hata katika mchakato wa uumbaji, Mungu anaonekana akisema! Kama watoto Wake, tumepewa uwezo sawa wa uumbaji kama Kristo kupitia maneno yetu. Biblia inasema maneno unayosema ni roho, tena ni uzima. Neno ‘ uzima ‘ katika tafsiri ya asili ni z ōé , likimaanisha uzima kama jinsi Mungu alivyo nao, au kwa maneno mengine, uzima unaomtia Mungu nguvu! Ndio maana maneno unayoongea hayawezi kufa! Ikiwa utasema, ‘ Mimi ni fukara ‘ maneno hayo yanazunguka, kutafuta njia za kufanya ungamo lako kuwa kweli!

Kinywa chako ni kituo cha uzalishaji wa kiroho. Chochote unachozungumza kinatafuta njia za kuthibitisha kile unachosema kuhusu maisha yako. Biblia inasema maneno mtakayosema hayatarudi kwenu bure, bali yatatimiza yote mliyoyatuma; kwa hiyo, ukinena maneno, PESA ZINAKUJA, itafanyika vile vile maneno yako yalivyotangaza!

## UKIRI WA KINABII

**Nina nguvu katika maneno yangu! Ninachagua kuzungumza mambo mazuri tu katika maisha yangu, bila kujali hali; mwili wangu una AFYA, mimi ni Tajiri wa ajabu katika Ufalme wa Mungu, Katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Isaya 55:11**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 14-15



**Waebrania 11:1**
**Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.**

Kinyume na wanavyoamini wengi, imani ni ya sasa! Maandiko yanasema, 'Sasa imani ni,' maana yake huwezi kutumia imani ya jana kwa leo. Ingawa imani hakika hujilimbikiza, inategemea hali uliyonayo sasa. Unafanya nini sasa? Je, unashikilia kile ambacho ni imani na kutii sheria zake? Neno ' bayana ' katika tafsiri asili hutafsiri moja kwa moja kua hypóstasis, ikimaanisha muundo mdogo au ukweli wa kimsingi unaokubaliana na yote mengine.

Imani hufanya kama hati miliki ya kile unachotaka kukipata na ndio uthibitisho na msingi wa unachokiamini. Kama Mkristo, umezaliwa katika imani lakini lazima ujifunze jinsi ya kuipata. Biblia inasema imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Mungu. Kwa hivyo, ili upate imani, lazima ulile Neno kila siku! Hakikisha unahudhuria kanisani na kusoma Neno la Mungu ili imani iongezeke ndani yako.

Zaidi ya hayo, Biblia inatuambia tuenende kwa imani na si kwa kuona, ikimaanisha imani inapaswa kufanya kazi kikamilifu bila kujali hali yako. Unapotembea kwa imani, umaskini hauna nguvu kwako, na hakuna ugonjwa wenye nguvu ya kukudhuru.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kutembea kwa imani katika kila eneo la maisha yangu! Ninapokula zaidi Neno la Mungu, imani inaongezeka ndani yangu, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Yakobo 2:26**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 16-18



**2 Wakorintho 12:4**
**Ya kuwa alinyakuliwa mpaka peponi, akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanamume ayanene.**

Kuna eneo fulani ambapo baadhi ya wanadamu wanaweza kukaribisha uwepo wa Mungu na kwenda zaidi ya mwanadamu wa kawaida. Unaweza kuwa bora kuliko wao katika unabii au hata uponyaji, lakini machoni pa Baba, wao ni roho bora zaidi! Paulo anaeleza uzoefu wake wa kwenda Mbinguni akisema alisikia maneno ambayo yalikuwa haijuzu kwake kuyatamka. Wale ambao ni roho bora zaidi husikia siri kutoka kwa ulimwengu mwingine!

Kuna viwango ambavyo vinaweza kufunuliwa tu kupitia kinywa cha roho zilizo bora zaidi! Ingawa hawaheshimiwi miongoni mwa makusanyiko ya watu, wanaheshimiwa na Mungu. Wanaume na wanawake hawa ni alama za uwepo wa Mungu kupitia Ukristo pekee!

Mungu amewafanya watumishi wake kuwa miali ya moto! Sharti la kuwa roho bora ni moto. Hii ina maana sababu ya adui zako kushindwa kukuangamiza ni kwa kukosa moto! Moto wa Mungu huzaliwa kwa kuwa na mazungumzo na Mfalme wa Wafalme na kutumia muda wa kujijaza na Neno Lake. Hebu fikiria uwezo ambao ungekuwa nao ikiwa tu ungetambua kwamba kuna moto unahitajika ndani yako, na unapokaribisha moto wa Mungu ndani yako, unakuwa roho bora zaidi!

## UKIRI WA KINABII

**Ninashikilia moto wa Mungu ndani yangu! Maisha yangu ni ishara kwa Kristo! Mimi ni mbeba uwepo wa Mungu katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Waebrania 1:7**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 19-21



**Zaburi 105:15**
**Akisema, Msiwaguse masihi wangu, wala msiwadhuru nabii zangu.**

Uhalisia wa kiroho unategemea uwezo wako wa kuhisi upako! Kuna njia fulani ambayo kila jemadari na mwangaza katika roho anaweza kujua upako ulipo. Watu wengi hata hawatambui kuna kitu kama kuhisi upako. Kwa sababu hii, kushindwa mara nyingi katika maisha yako kunaweza kuchangiwa na kutotambua upako wa watu ambao Mungu aliwatuma kukusaidia.

Unapoendelea na mwendo wako katika Kristo, ni muhimu kwamba uheshimu na kuhisi upako kwa wale ambao Mungu amewachagua na kuwaweka katika mamlaka juu yako. Katika Biblia, tunaona pepo akilazimishwa kuhubiri Paulo alipokuwa akipita kwa sababu ya nguvu nyingi ambazo mtume huyo alikuwa nazo ndani yake. Hii ina maana shetani pia anaweza kunusa, kugusa na kuhisi upako.

Kataa kuruhusu maneno ya wengine yaongoze maisha yako! Hasa ikiwa maneno hayo ni kinyume na kile Mungu anasema kuhusu maisha yako. Inaweza kuonekana kama bosi wako, mwalimu, au mfanyakazi mwenzako anakunyanyasa kwa sababu ambazo hujui, lakini ni kwa sababu wanatishiwa na upako wanaouhisi ndani yako!

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kutambua ni nani Mungu amemtuma kunisaidia! Nimepewa roho ya utambuzi; Sitamtegemea mtu yeyote kuhisi upako wa Mungu, katika Jina Kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Yohana 2:20**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 22-23



**Yohana 3:16**
**Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.**

Nini kilisababisha Mungu kuondoka Mbinguni ili akusamehe? Kwa nini kupitia mchakato wa kutafuta mwili wa mwanadamu, kuwa kiinitete, kusubiri miezi tisa, kukua hadi utu uzima na hatimaye kufa msalabani, kisha kuwasamehe watoto wake. Je, unatambua Mungu alichukua sura ya mtumwa na akaondoa Uungu ili tu aje hapa na kukusamehe!

Kwa nini shetani hajatubu hadi leo, lakini anaelezewa kuwa ndiye upeo wa ukamilifu, kwa maneno mengine, kiumbe mwenye akili zaidi. Je, unafikiri kweli shetani hajahesabu alichopoteza hadi sasa? Sababu ya hii ni roho haiwezi kusamehe! Kwa macho ya roho, msamaha unaweza tu kutimizwa wakati kifo kinapotokea. Hii ndiyo sababu Mungu alimtuma Mwanawe, Yesu Kristo, kufa kwa ajili yako ili upate kusamehewa!

Tambua, katika Biblia ni mawazo ya shetani ndiyo yalimfanya aondolewe kutoka Mbinguni. Hakuwahi kutekeleza au kutendea kazi mawazo haya! Ibilisi anakuchukia kwa sababu unatenda dhambi kila siku, lakini Mungu anaendelea kukupenda na kukusamehe!

## UKIRI WA KINABII

**Nimesamehewa dhambi zangu zote; Mungu alimtuma Mwanawe ili nipate kusamehewa na kuishi maisha yanayotoririka maziwa na asali. Utukufu ni kwa Mungu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 86:5**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 24-25



**2 Timotheo 3:16**
**Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.**

Sarafu na pesa ni vitu viwili tofauti. Sarafu hupima thamani ya ubadilishaji ilhali pesa ndiyo hifadhi yake. Leo, pesa haipewi thamani na chochote. Ile iliyokuwa sarafu iliyowahi kutumika duniani kote (dola) inaendelea kupungua thamani! Ambapo hapo awali ilikuwa inapewa thamani na dhahabu, sasa ni maneno yetu ambayo yanaipa thamani pesa! Hii ina maana pesa pia inaweza kuamriwa na kudhibitiwa kwa nguvu ya maneno yako! Kila Mkristo amechukua urithi wa Ki-Mungu katika Kristo Yesu, ikimaanisha kama mtoto wa Mungu, umaskini hauna chaguo ila kufunga virago!

Sarafu lazima iwe ya kubebeka, kudumu na inagawanyika. Unapoongeza thamani yako, pesa nyingi huja ili kuhalalisha thamani hiyo. Hudhuria kikamilifu kwenye kusoma Neno la Mungu, kama vile Biblia inavyosema kwamba usomaji wa Neno una faida katika sehemu zote za maisha yako. Mungu ni Mungu wa kuzidisha; Hawezi kuzidisha chochote kwa sifuri. Ni lazima ujitengenezee thamani ili Mungu akutumie na kukuzidisha. Chagua kujihusisha na watu wenye nia moja ambao hawaondoi bali wanaongeza thamani kwenye maisha yako!

## UKIRI WA KINABII

**Pesa inakuja kwangu! Fedha zangu zitapata kimo cha anga! Wale walionidharau, watanitazama juu kwenye maziwa na asali yangu, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Yohana 10:10**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Mambo ya Walawi 26-27



**Yohana 14:30**
**Mimi sitasema nanyi maneno mengi tena, kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu.**

Tatizo la watu duniani leo ni kwamba hawatambui kila mtu anatoa nishati! Hakuna njia kwa ushawishi wowote wa mapepo kuingia katika maisha yako isipokuwa utoe kitu kinachowavutia. Yesu alimwona shetani akasema hakuna hata sifa moja aliyoshiriki naye! Kwa maneno mengine, mtu anaweza kuruhusu mashambulizi kadhaa ya shetani kwake kupitia tabia zake mwenyewe zinazotoka ndani yake.

Wanasayansi hivi karibuni wamegundua kuwa mwanga na maada vinategemeana, kwani huwezi kuwa na mwanga bila maada na maada bila mwanga. Wazo hili la chanzo na matokeo linaonyesha sababu ya wewe kuwa jinsi ulivyo ni matokeo ya vitu viwili kuwa tegemezi na kuitikiana!

Sababu ya Mungu kudai utakatifu ni kwa sababu utakatifu huzuia uzalishaji wowote unaoweza kumvutia shetani! Kama mtoto wa Mungu, kataa kukubali tabia zozote za shetani maishani mwako. Usikubali magonjwa, umaskini au hasira. Acha wito wako ukusukume na kuelekeza maisha yako ili uzalishaji wako uondolewe kutoka kwenye kufikiwa na shetani!

## UKIRI WA KINABII

**Sina kabisa tabia za shetani ndani yangu! Ninaakisi wema wa Mungu katika kila jambo ninalofanya; mimi ni mtakatifu na nimetengwa. Wito wangu ndio fokasi yangu pekee, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Warumi 8:29**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 1-2



**Wagalatia 2:20**
**Nimesulubiwa pamoja na Kristo; Lakini ni hai, wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.**

Kama mtoto wa Mungu, umesulubishwa pamoja na Kristo! Ukiwa umekufa katika mwili, hauishi, bali Kristo yu hai na anapumua kupitia kwako. Hii ina maana kwamba Biblia inasema kwamba wanapokuona, wamemwona Kristo! Mara tu unapofahamu dhana hii na kuendelea nayo kama ukweli wako katika Kristo, hufanyi makosa! Hakuna kitu kinachoitwa ugonjwa au umaskini kwa sababu Yesu hasumbuki na magonjwa au umaskini. Wale ambao wamekufa katika mwili hawajali watu wengine wanafikiri nini au wanasema nini!

Unapoishi maisha ya kusulubiwa, lazima usulubishe mwili kila siku! Mwili una tamaa zake wenyewe ambazo lazima uzichome moto; ziue tamaa za mwili kabla hazijakuua wewe. Kama Mkristo, Mungu amekuumba na kukuweka kuwa jinsi Kristo alivyo. Tembea katika mtazamo huu, nawe utafanya mambo makuu katika Ufalme wa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha ya kusulubiwa! Nimekufa katika mwili na ni hai kupitia Yesu Kristo! HAKUNA aina yoyote ya ugonjwa inayoweza kuniangamiza. Tamaa zote za mwili zimezikwa, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Warumi 8:13**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 3-4



**Marko 16:17**
**Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya.**

Kila Mkristo amepewa uwezo wa kuwa mtaalamu wa kuangamiza pepo! Ingawa Mungu alitupa uwezo wa kutoa pepo kwa jina lake, Wakristo wengine bado wanateswa na kila aina ya magonjwa na mambo kama hayo. Sababu ya hii inaweza kuhusishwa na Wakristo wengi kutumia jina la Mungu lakini si tabia yake. Neno ' jina ' katika tafsiri yake ya asili ni ónoma, likimaanisha tabia.

Biblia inazungumza kuhusu wana saba wa kuhani mkuu wa Kiyahudi kujaribu kutoa pepo kwa jina la Yesu na kushindwa! Kwa kweli hawakuwa na tabia ya Yesu ya kuunga mkono walichokuwa wakisema. Usikubali hila za shetani au kumruhusu aingie katika maisha yako, kwa maana Biblia inasema Mungu amewapa ninyi mamlaka juu ya kila uovu na uwezo wa kukanyaga nyoka. Chagua kutembea katika tabia ya Kristo katika kila jambo unalofanya. Inoe akili yako kupitia Neno la Mungu ili kufanana zaidi na Kristo. Unapotembea katika tabia ya Yesu, hakuna chochote kitakachokudhuru!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni MTAALAM WA KUANGAMIZA MAPEPO! Hila za shetani hazitanidhuru wala kunidanganya. Nakataa magonjwa; Nina uwezo wa kushinda chochote na hakuna kitakachoniumiza kwa Jina la Yesu! Amina..**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Luka 10:19**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 5-6



**Waebrania 12:22**
**Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi.**

Macho yako yanapokuwa hayajafunguliwa kwenye ulimwengu wa roho, unaruhusu matatizo kadhaa kuingia katika maisha yako. Kama Mkristo, kuona malaika kunapaswa kuwa jambo la kawaida katika maisha yako! Unapotazama utendaji wa jicho, unaweza kuona kwa kuzingatia miale ya mwanga inayoakisi kutoka kwenye kitu na kuingia ndani ya macho kupitia konea (safu ya uwazi ya nje inayofunika jicho). Kiasi cha mwanga kinaratibiwa na mboni. Hatimaye, mawimbi hutumwa kwa zaidi ya vihisi milioni 125 kwenye retina, kukuwezesha kuona. Hebu fikiria kwamba kuona kwako kunategemea tu mwanga unaoingia machoni pako!

Biblia inatuambia kuingia kwa Neno la Mungu hutupatia nuru. Maana yake ni kwamba ili uwaone malaika ni lazima usome maandiko yanayowahusu malaika ili nuru ya malaika iingie ili uwaone! Mungu aliumba malaika kukusaidia na kukuwezesha! Unaporuhusu mara kwa mara nuru ya malaika kukuingia, kuona malaika litakuwa jambo la kila siku!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaona malaika kila mahali ninapoenda! Ninaposimama hapa sasa, kuna idadi isiyohesabika ya malaika pamoja nami! Ninaposoma Biblia yangu, nuru inaniingia, katika Jina la Yesu! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 119:130**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako kwa ajili ya leo: Hesabu 7



**Ufunuo 1:10**
**Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana, nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu.**

Haiwezekani kuwa katika Roho bila kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Bwana. Kuna Wakristo wengi sana ambao hawasikii sauti ya Mungu, wanaotumia vibaya maneno, sauti na akili zao wenyewe ili kuwa ' sauti ya Mungu. 'Utakuta wakiomba kazi na kukataliwa, wanasema haikuwa mapenzi ya Mungu wao kupata hiyo kazi, na wakikubaliwa, wanasema yalikuwa ni mapenzi ya Mungu! Biblia inatuambia Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza. Kwa sababu tu matukio fulani yanaonekana kwa njia fulani haimaanishi Mungu alizungumza au hakuzungumza. Jifunze kuongozwa na Roho wa Mungu. Jifunze kutembea na kufanya mambo katika Roho.

Usiwe kama wale wanaotabiri maono kwa tamaa zao wenyewe badala ya maono na ndoto za Mungu. Una misheni maishani mwako ambayo lazima uuchukulie kwa uzito. Kwa hivyo, usiongozwe na sauti za wengine, haswa wale walio wa ulimwengu. Kuwa na nidhamu ya kutosha kusikiliza sauti ya Roho wa Mungu, na kuruhusu Mungu awe dereva wako!

## UKIRI WA KINABII

**Naisikia sauti ya Roho wa Mungu; hakuna hali inayoweza kunichanganya! Kila uamuzi ninaofanya unaongozwa kabisa na Roho wa Bwana. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 143:10**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 8-9



**1 Yohana 5:4**
**Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu, na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.**

Kila Mkristo mmoja mmoja anapaswa kutembea katika mawazo ya ushindi. Wazo kama vile kutofaulu linapaswa kuwa geni akilini mwako. Mtu anayemiliki silaha yenye nguvu zaidi duniani na hajui jinsi ya kuitumia ndiye mtu dhaifu zaidi duniani. Hivi ndivyo watoto wengi wa Mungu wanavyoendesha maisha yao, lakini tayari mmeushinda ulimwengu huu!

Biblia inasema hatukosi kuzijua hila za shetani. Hana mamlaka yoyote juu yako kama mtoto wa Bwana. Hakuna silaha yenye nguvu ya kukuangamiza ambayo imewahi kutengenezwa au itakayowahi kufanywa! Wewe ni mtoto wa MFALME!

Haijalishi unapitia nini leo, kuna tiba ndani ya Neno la Mungu! Wale wote wanaopigana dhidi yako wanapigana vita ya kushindwa. Umefanywa kuwa mshindi katika Kristo; kama mtoto wa Mungu, ushindi ni urithi wako! Acha kutofaulu kuwa dhana isiyowezekana! Kuwa na mtazamo wa ushindi katika kila jambo unalofanya, mtazamo wa maziwa na asali; na utaona jinsi maisha yako yatakavobadilika kabisa!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mshindi katika Kristo Yesu! Kifo, magonjwa au zana nyingine yoyote ya shetani haina madhara kwangu wala kwa familia yangu! Katika mwaka huu, nitapata ushindi usio na kifani, katika Jina Kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Kumbukumbu la Torati 20:4**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 10-11



**Yohana 10:34**
**Yesu akawajibu, Je! Haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba, Mimi nimesema, Ndinyi ni miungu?**

Miungu huwasiliana na miungu! Hii ndiyo sababu Mungu alikaa kimya; Hakuwa na mtu mwingine wa kuzungumza naye. Hata ukimwangalia mungu wa dunia hii (shetani), katika kitabu chote cha Mwanzo, hatuoni akiongea mpaka alipomuona Adamu! Hii ina maana kuwa Adamu alikuwa ni nakala kamili ya Mungu! Unapoanza kupiga mbizi katika ulimwengu wa ndani zaidi katika Kristo, lazima uangalie ni nani unayemruhusu akufikie. Hakikisha wale wanaokuzunguka wanaelewa kiwango cha ufunuo ulionao na safari iliyokuchukua rohoni kufikia hatua uliyopo.

Kama mungu, lazima uelewe wewe ni nani! Katika ulimwengu wa leo, watu huenda kwenye makaburi na kupata mawe ya kaburi ya Waislamu, Wahindu na Wakristo karibu na kila mmoja. Sababu ya hii ni kwamba Wakristo wengi hawafikii utambuzi wa wao ni nani katika Kristo! Wakristo ni miungu na, kwa hiyo, hawapaswi kufa kama wanadamu tu. Ndege huzaa ndege, na simba huzaa simba! Wewe ni mtoto wa Mungu aliye juu; wewe ni mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni Mungu sirini! Nimezaliwa na Mungu kwa hiyo kifo hakina nafasi katika maisha yangu! Hakuna kitakachonizuia mwaka huu! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Zaburi 82:6**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 12-13



**Warumi 1:1**
**Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa ahubiri Injili ya Mungu**

Katika siku za kale katika Israeli, baada ya miaka saba, mtumwa alistahili uhuru wake. Hata hivyo, mtumwa anapoamua kwa hiari kubaki katika nyumba ya bwana wake na kutomwacha aishi maisha ya uhuru wake mwenyewe, basi sikio lake hutobolewa, na anaendelea kufanya kazi katika nyumba ya bwana wake akiwa "mtumishi mtumwa" au "MTUMWA". Kwa hivyo, Paulo anasema amejitolea kabisa kumtumikia Kristo bila kulazimishwa.

Paulo anasema, nilikuwa mtumwa niliyepewa uhuru wa kumwacha bwana wangu, lakini kwa sababu bwana wangu ni mwema sana kwangu, siwezi kumuacha. Nimejitolea kwa nafsi yangu yote kumtumikia Yeye! Ni wangapi kati yetu wanaweza kusema kwa dhati kwamba hiyo pia ni kweli kwangu: Niko tayari kwa kila kitu kumtumikia Bwana wangu Yesu; Nitaenda kumtumikia si kwa kulazimishwa bali kwa hiari na kwa furaha? Wema wa Bwana ni mwingi wa nguvu na unaendelea kutiririka bila kujali mapungufu yetu. Jihesabu kuwa MTUMWA katika shamba lake la mizabibu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninayatoa maisha yangu upya kwa Yesu, Mfalme, Bwana na Mwokozi wangu. Ninatoa maisha yangu yote kwa ajili Yako, Bwana; tayari kutumika kama rungu Lako la vita kuleta mabadiliko katika kipindi hiki cha mwisho, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**1 Wakorintho 1:1**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 14-15, Zaburi 90



GoodNews DAILY



**Mwanzo 1:2**
**Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu; na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji**

Andiko linaonyesha kwamba dunia kama tunavyoijua sasa ilikuwa na "ukiwa" na "utupu" tangu mwanzo. Utupu hapa unajumuisha utupu, kutokuwa na kitu, kama nyika ambayo hakuna kinachotarajiwa kukua! Wakati Roho wa Mungu " alipotulia " , tafsiri ya Kiebrania ya andiko hilo ni " rachaph " , ikimaanisha kuzaa kwa kutafakari daima juu ya matokeo. Ilikuwa hapo na ndipo kitu kipya kilizaliwa. Roho Mtakatifu alikuwa akiatamia au kuangua, kisha hatimaye akasema, "na iwe Nuru", na kukawa na nuru!

Kuatamiwa kiroho kuna masharti ikiwa unataka matokeo yawe kama ilivyokusudiwa. Kupanda na kushuka kwa joto huathiri sana matokeo. Kwa hiyo, wakati kuatamiwa kiroho kunapofanyika, anza kuinua kiwango cha tabia yako, ongeza maisha yako ya maombi, ongeza kiwango cha ibada yako kwa Mungu na uone maisha yako yanakuwa ya ajabu. Mchakato wa katamiwa kwa kiroho huharakisha ukuaji wako wa kiroho na kuruhusu uwezo wa kiroho kujengwa. Kwa hivyo, panua ushirika wako na Roho Mtakatifu ili kukuwezesha kuishi upya wa maisha kwa njia isiyo ya kawaida.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni uzao mpya! Nimezaliwa kwa Roho, na hakuna kinachoweza kunizuia kutimiza kusudi langu nililopewa na Mungu. Mwangaza wa maisha yangu utaangazia kila kitu kinachonizunguka kwa utukufu wa Mungu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 4:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 16-17



**Isaya 54:17**
**Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa; na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa Mungu Bwana, na haki yao inayotoka kwangu, asema BWANA**

Leo, ninaamuru na kutangaza Neno la Bwana kwenu kama ilivyoelezwa kwa makusudi katika Isaya 54:11-17: "Ewe uliyeteswa, uliyerushwa na tufani, usiyetulizwa, tazama, nitaweka mawe yako kwa rangi nzuri, nitaweka misingi yako kwa yakuti samawi. Nami nitaifanya minara yako ya akiki nyekundu, na malango yako ya almasi, na mipaka yako yote ya mawe yapendezayo. Na watoto wako wote watafundishwa na BWANA; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi!

Utathibitika katika haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwa maana hutaogopa; na mbali na hofu, kwa maana haitakukaribia. Tazama, yamkini watakusanyana; lakini si kwa shauri langu. Watu wo wote watakaokusanyana juu yako wataanguka kwa ajili yako.

Tazama, nimemwumba mhunzi afukutaye moto wa makaa, akatoa silaha kwa kazi yake; nami nimemwumba mharibu ili aharibu. Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa BWANA, na haki yao inayotoka kwangu mimi, asema BWANA.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yamewekwa kwa ajili ya mafanikio; Siwezi kushindwa! Mungu alisema, Nabii alisikia, hilo latosha! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Danieli 3:26

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 18-20



**Matendo 12:9**
**Akatoka nje, akamfuata; wala hawakujua ya kuwa ni kweli yaliyofanywa na malaika; bali alidhani kwamba anaona maono.**

Kufunguliwa Petro kutoka gerezani kulikuwa ni uingiliaji kati wa Ki-Mungu ulioratibiwa na malaika. Jambo la kupendeza ni kwamba mchakato ulipokuwa ukiendelea, Petro hakuamini kilichokuwa kikitendeka. Kwa kweli, katika kujaribu kuchakata mwingiliano kati ya hali ya asili na hali ya Ki-Ungu katika kuingia na kutoka, Petro alihitimisha kwamba ilikuwa ni maono, akikataa kukubali ukweli kwamba sasa alikuwa nje ya gereza!

Leo, nazungumza na hali hiyo ya utasa katika ndoa yako, fedha zako, kazi yako, huduma yako, kwamba wakati wako wa ukombozi ni sasa! Kama Petro, itaonekana kama ndoto kwako kwa sababu inafanyika kwa haraka na kwa haraka sana kiasi kwamba uwezo wako wa kufikiri utakuwa si kitu. Muujiza huu ninaokutangazia sasa ni zaidi ya ufahamu wa kibinadamu: fedha zako zinasukumwa kutoka ulimwengu wa roho, pesa zako ziko karibu kudhihirika, na ushuhuda wako wa maziwa na asali utakushtua. Ukweli mpya wa utele umekuja kwako. Sio ndoto; huu sasa ni uzoefu wako mpya katika Kristo. Maisha yako ya kifungo yamekwisha, na hayatakutembelea tena kamwe!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni Kito cha Mungu, nimeumbwa kwa njia ya ajabu ili nionyeshe utukufu na fahari Yake. Mwonekano wangu wa Kifalme unaonekana. Ngome za ufukara na uhaba zinabomolewa sasa kwa Jina kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 126:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 21-22



**Isaya 43:18**
**Msiyakumbuke mambo ya kwanza, wala msiyatafakari mambo ya zamani.**

Kila mbegu ina kifuniko au koti inapopandwa ardhini, na huko, chini ya ardhi, mbegu hufukiwa, lakini ni msimu tu wa mbegu. Hata hivyo, hata katika hali hiyo, kuna mto ulioifunika mbegu. Mkristo hapaswi kamwe kufikiria kwamba amesahauliwa! Unaweza kuhisi umezikwa chini ya matatizo mengi ambapo inaonekana umuhimu wako umesahaulika, ujuzi wako umezikwa, miunganiko yako imekatika, fedha zako hazipo, na familia yako inasambaratika. Matatizo yako yanarundikana moja baada ya jingine, na inaonekana hakuna njia kwako!

Ninaleta habari njema kwako sasa hivi: hauko peke yako; hujasahaulika. Kama mbegu iliyozikwa chini ya ardhi, ni suala la muda tu kuona mbegu hiyo hiyo ikiota na kudhihirisha upya kwa mshangao wa wapita njia na furaha ya Mkulima. Mchana umefika licha ya msimu wako wa usiku. Kwa hakika kama Bwana aishivyo, familia yako haitasambaratika, biashara yako haitaanguka, na ugonjwa huo hautakutoa nje. Msimu wako wa kuota ni sasa! Utashuhudia hili hakika, maziwa na asali ndicho unachokiishi mwaka huu; furahi milele!

## UKIRI WA KINABII

**Katika uso wa dhiki, imani yangu kwa Mungu haitapungua. Mimi ni zaidi ya mshindi; ushindi baada ya ushindi, ninashinda kila kitu kinachonijia! Utukufu kwa Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 23-25



**Yakobo 1:24**
**Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.**

Maneno na maoni ya Wakristo nyakati fulani ni ya kutatanisha. Watasema mambo kama vile, "Mungu ananishughulikia, kwa hivyo sina budi kupitia ugumu huu" , au " Mungu ananiadhibu kwa kipandauso hiki " . Huu ni wazimu tu! Hakuna namna Mungu atapata utukufu katika kushindwa kwako! Hakuna namna ambayo Mungu anakufundisha somo kwa kukupa magonjwa; hapana, huyu si Mungu. Mungu kamwe hatumii zana za shetani kuwafundisha watoto wake masomo. Mungu hakufundishi somo kwa kuweka mambo hasi katika maisha yako, la! Mungu hatumii mbinu za adui kuendesha ajenda yake.

Unawajibu wa kuorodhesha aeons zako pekee. Kusiwe na mtu au kitu cha kulaumiwa kila wakati unapokuwa huoni maendeleo katika maisha yako! Kujichunguza ni muhimu. Jiulize, Je, ninautumiaje muda wangu? Je, nipo makini na zaka zangu? Je, nina nidhamu na kuendana na maisha yangu ya maombi? Je, ninachukua kusoma neno la Mungu kwa uzito? Unapoanza kufanya mambo kwa njia tofauti, hakika matokeo tofauti yatakujia; anza kuifanyia mazoezi leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni sanaa ya Mungu, spishi mpya ambayo haijawahi kuwepo hapo awali. Sikati tamaa wala siachi, na nina imani kwamba nitashuhudia hivi karibuni! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 1:66

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 26-27



**Waefeso 1:3**
**Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho,ndani yake Kristo.**

Maandiko yetu ya leo yanahusisha kuelewa "baraka zote za rohoni". Mungu, katika nguvu zake kuu, aliamua kutuletea "baraka zote za rohoni" kupitia Yesu! Ninamaanisha Yule anayeketi katika mzingo Wake Mwenyewe alifanya uamuzi wa kutubariki kwa "baraka zote za rohoni" katika Kristo! Ukifikiria juu yake, Mungu, kwa ukarimu wake, alijitwika jukumu la kutubariki bila kujali mapungufu na kasoro zetu! Ndiyo maana huwa nasema Mungu hakukasirikii; Ana hasira tu kuhusu wewe!

Jambo moja ambalo naamini sasa unaelewa ni hili: maisha ni ya kiroho! Kwa hiyo, Mungu alipoamua kutubariki kwa baraka za kiroho katika Kristo, alionyesha wema wake kwetu kwa kiwango cha juu zaidi. Unapokuwa na Kristo, una baraka zote za kiroho - si baadhi, lakini zote. Hesabu 23:20 inaiweka hivi, "Tazama, nimepewa amri ya kubariki, Yeye amebariki; nami siwezi kulitangua." Chochote wanachosema au kufikiria juu yako hakina umuhimu wowote. Anachosema Mungu juu yako ndio kipaumbele. Alisema mwaka huu ni mwaka wako wa maziwa na asali; hilo linaweka mambo sawa!

## UKIRI WA KINABII

**Nimebarikiwa na kupendelewa sana; Siwezi kupuuzwa. Maisha yangu ni maisha ya furaha na amani. Mimi ni hazina ya Mungu, yenye thamani zaidi ya marijani. Yeyote anayenigusa, amekwisha!**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 28-30

## ULIMI AMBAO NI BUNDUKI



**Yohana 6:63**
**Roho ndiyo itiayo uzima; mwili haufai kitu; maneno hayo ninayowaambia, ni roho, tena ni maisha.**

Unahitaji msimbo wa pande mbili ili kuwasiliana katika ulimwengu wa Roho. Roho hazizungumzi lugha zako zinazojulikana kama Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa au Kijerumani. Roho huwasiliana kwa ishara na alama. Kuna aina za lugha, ndimi fulani unazoomba, ni kama vile kufyatua bunduki na kurusha makombora ya masafa marefu katika ulimwengu wa Roho, na kusababisha uharibifu katika kambi ya adui. Jione kama kitovu cha nguvu, kituo cha nyuklia kinachokusudia kuangamiza ngome yoyote ya adui.

Adui anaendelea kukunyanyasa kwa sababu anadhani wewe ni mtu dhaifu na wa kawaida. Sasa inuka, shikilia ghala lako la silaha lililowekwa katika ndimi zako, na uanze kupiga kelele, mlipuko, na kuponda kwa ndimi zako za bunduki. Sasa ni wakati wa vita. Katika mwaka huu wa maziwa na asali endelea kumshambulia adui mpaka amani yako irudishwe, fedha zako zirudishwe, na nyumba yako irudi kuwa sawa. Sukuma ndimi zako kwa kiwango kingine; usiache mpaka uchukue kilichochukuliwa kutoka kwako.

## UKIRI WA KINABII

**Ulimi wangu ni kama kalamu ya mwandishi stadi. Sauti yangu italeta misukosuko katika kambi ya adui. Mimi ni jeshi la mtu mmoja; pamoja na Yesu, ninateka himaya. Mwaka huu, nitahama kutoka ushindi hadi ushindi katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Yohana 5:21**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 31-32



**Yohana 6:68**
**Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana, twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele.**

Kauli hii iliyotolewa na Simoni Petro inaashiria mambo mengi sana. Simoni Petro na wanafunzi wengine wameweka wazi utafiti na matokeo yao: ni Yesu pekee aliye na "Maneno ya uzima wa milele". Yohana 1:1 inasema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Mstari wa 14 wa sura hiyo hiyo unasema, "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli." Yesu ndiye NENO aliyedhihirishwa katika mwili!

Tambua kwamba Yesu ni Mungu, kwa hiyo maneno ambayo Mungu anazungumza ni ya milele. Huo ni ukweli! Yesu anasema katika Marko 13:31, "Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe." Maneno ya Yesu ni ya milele na yatastahimili majaribu ya muda! Unapokuwa na maneno ya uzima wa milele ya kukuendesha, magonjwa yatakukimbia. Unapozungumza, akaunti yako ya benki kama kiumbe itajibu. Unachobeba ni cha milele na chenye nguvu na kinahitaji kujifunua katika maisha yako ya kila siku!

## UKIRI WA KINABII

**Umilele na Uungu unakaa ndani yangu; kwa hiyo, ninatembea kwa nguvu. Ninapozungumza, ninadhihirisha umiliki. Maisha yangu ni maisha ya ubora; mazingira yangu yamejaa miujiza, ishara na maajabu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 16:16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 33-34



**Zaburi 92:12**
**Mwenye haki atasitawi kama mtende; Atakua kama mwerezi wa Lebanoni.**

Tazama kustawi kwa mwenye haki kunafananishwa na mtende. Kuna kitu cha kipekee kuhusu mtende ambacho wenye haki wanaweza kufananishwa nacho. Kuna sifa fulani za mtende ambazo tunapaswa kuiga. Mtende ni rahisi kupindika na kustahimili dhoruba! Mtende unaweza kujipinda nyuma, mbele, na pembeni katika uso wa dhoruba kali bila kuvunjika. Bado baada ya dhoruba, mtende bado unakuwa umesimama, hauwezi kutikiswa, na thabiti.

Kulinganisha mtende na mwenye haki - Mkristo - kama inavyoonyeshwa katika maandiko ya leo sio bahati mbaya. Katika uso wa dhiki, Mkristo anatarajiwa kusimama imara. Katika kukabiliana na changamoto za maisha, kama dhoruba za maisha, Mkristo hapaswi kuyumba bali kusimama imara katika Neno la Mungu, akiwa amejikita katika imani. 2 Wakorintho 4:8-9 inatangaza, "pande zote twadhikika,bali hatusongwi; twaona shaka bali hatukati tamaa, twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini bali hatuangamizwi." Unatoka kama maziwa na asali!

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yatakuwa maajabu! Dhoruba itakapokwisha, nitabaki nimesimama imara. Maisha yangu yamefichwa ndani ya Kristo; Siwezi kuangamizwa, sitaenda chini, lakini simama wima kutangaza Neno la Mungu! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Hesabu 35-36



**1 Wathesalonike 4:16**
**Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu...**

Tuna faida ya kipekee inapokuja kwa huduma kwa sababu ya ufunuo ambao tumepokea kutoka kwa Mungu. Huu ni mwonjo wa utukufu wa Ki-Mungu. Andiko liko wazi, lakini nadhani ninahitaji kufafanua juu ya hili. Bwana, siku hiyo, akishuka kutoka Mbinguni, atapiga kelele kwa sauti ya malaika mkuu. Wafu katika Kristo watafufuka kwanza watakaposikia tarumbeta ya mwisho. Hii ina maana ni sauti ya malaika mkuu pekee inayoweza kusikika na wafu na kuwafufua!

Mara nyingi huwa natangaza, " Kwa sauti ya malaika mkuu ", kwa sababu sauti ziko tofauti, na wanaume na wanawake wa Mungu wako tofauti. Kuna mvuto wa Roho unaokuvuta kwa wale wanaoteseka na wenye uhitaji. Leo, natamka kwa sauti ya malaika mkuu kwenye tumbo la uzazi lililokufa, kwenye ndoa hiyo iliyokufa, kwa kampunii ile iliyokufa, kwenye akaunti hiyo ya benki iliyokufa ili kufufuka sasa na kuanza kuzaa matunda na kuzalisha. Mauti imefukuzwa kutoka kwenye maisha yako sasa!

## UKIRI WA KINABII

**Sauti yangu itatawala mawimbi ya hewa, na kwa sauti yangu, pesa yangu itanisikia bayana. Ninaamuru na kutangaza kwamba sitafilisika kamwe siku nyingine katika maisha yangu! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 24:31

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 1-2



**Zaburi 82:5**
**Hawajui, wala hawafahamu; hutembea gizani: Misingi yote ya nchi imatikisika.**

Mmoja wa watu wenye nguvu zaidi lakini mara nyingi hupuuzwa katika Biblia ni Adamu! Anguko la Adamu liliunda vurumai katika anga za mbinguni kiasi kwamba ulimwengu wote, mifumo ya dunia, na mwezi na nyota zilikosa mpangilio. Biblia inatuambia kwamba Yesu ndiye Adamu wa mwisho: "Ndivyo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi hai; Adamu wa mwisho akawa roho yenye kuhuisha." (1 Wakorintho 15:45,). Kwa hiyo, unafikiri Adamu wa kwanza hakuwa na uwezo? Hapana, bwana!

Katika bustani ya Edeni, Adamu alipata taarifa kutoka kwa mti, na leo, hata tunapata dawa kutoka kwenye miti. Pesa hufanywa kutoka kwenye karatasi, ambazo hufanywa kutoka kwenye miti. Kwa hiyo ikiwa Adamu angekula kwanza kutoka kwenye mti wa uzima, wanadamu hawangekuwa wagonjwa! Mamlaka na utawala wa Adamu unazidi sana ule wa kawaida. Adamu alipoteza mamlaka hayo alipoasi, lakini Adamu wa mwisho, Yesu Kristo, alirudisha nguvu na mamlaka hiyo kwetu. Sasa unaweza kuzungumza na mazingira na mazingira yako, na hayana chaguo ila kutii na kuona mabadiliko yakitekelezwa!

## UKIRI WA KINABII

**Ninarejeshwa kwenye uwezo katika Kristo. Ninazungumza maneno yanayoumba, ninabeba DNA ya Mungu, mimi ni wa ufalme, na uumbaji ni watumishi wangu. Nitatawala, na kushinda ndilo nifanyalo! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 11:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 3-4



**Ufunuo 4:7**
**Na huyo mwenye uhai wa kwanza alikuwa mfano wa simba; na mwenye uhai wa wa pili alikuwa mfano wa ndama; na mwenye uhai wa tatu alikuwa na uso kama uso wa mwanadamu; na mwenye uhai wa nne alikuwa mfano wa tai arukaye.**

Mmoja wa wale viumbe wanne walioketi kukizunguka kiti cha enzi cha Mungu alikuwa na uso wa mwanadamu. Kwa hiyo, kwa kweli, mwanadamu alikuwa pamoja na Mungu kabla ya kuumbwa kwa Adamu, lakini ona sifa ya kustahili: Mungu alisema na tuumbe "mtu kwa mfano wetu". Hilo linatujulisha kwamba Adamu kama mwanadamu aliumbwa tofauti na kiumbe kilichokuwa na uso wa mwanadamu. Mungu alituumba kwa mfano wake tukiwa na roho, nafsi na mwili. Mwili ulifanywa kwa udongo, hivyo mwili au nyama ni wa kimwili.

Ibilisi alipomshawishi Hawa kula matunda ya mti uliokatazwa, naye akamshawishi mumewe kufanya vivyo hivyo, laana iliwekwa juu ya nyoka kwamba atakula mavumbi (Mwanzo 3:14). Walakini, sote tunajua nyoka hawali vumbi. Kwa hivyo, 'vumbi ' hili linarejelea nini haswa? Inaashiria mwili. Adui hushambulia mwili, kwa hiyo ni muhimu kuilisha roho yako kila siku kwa Neno la Mungu ili kuzishinda tamaa za miili yetu. Endelea kuthibitisha maziwa na asali hata kwenye maisha yako ya kiroho na itakuwa hivyo.

## UKIRI WA KINABII

**Ninakua rohoni mwangu kwa Neno la Mungu. Ninajenga upinzani dhidi ya mishale yenye moto ya adui. Ninao ujasiri wa kiroho wa kumfanya adui akimbie kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Ezekieli 1:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 5-7



**Marko 10:27**
**Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yanawezekana kwa Mungu.**

Kuna uwezekano usio na kikomo katika ulimwengu wa Roho. Biblia inaposema mambo yote yanawezekana kwa Mungu, inamaanisha "mambo yote"! Hakuna ubaguzi inapokuja kwa uwezekano kwa Mungu. Kumbuka kwamba mambo mengi katika Roho hayafundishwi bali yanashikwa! Jambo moja muhimu unapaswa kujua leo ni kwamba kupata vitu vya Roho kunahitaji gari. Magari mengine yanaweza kuwa ni binadamu! Mazingira fulani yanaitwa magari katika Roho kwa sababu yanakusukuma hadi mahali ambapo hatima yako itazaliwa.

Unapopata gari lako, utachukuliwa kutoka eneo moja hadi jingine na kuona maendeleo katika maisha yako. Unapochagua gari sahihi, utainuka na kusherehekewa. Baadhi ya shida husababisha kupanda,bila kukusudia, pia huwa magari yanayokupeleka kwenye kiwango chako kinachofuata. Hiyo hali uliyoita ni kifungo ambacho kimesumbua ndoa yako, fedha, wizara au watoto ndio gari litakalokusafirisha hadi ikulu yako. Usiogope; pitia hayo.

## UKIRI WA KINABII

**Nimepanda juu ya upepo wa magari ya vita; misukosuko inaweza kuja kutoka nyuma, lakini inanisukuma tu kwa msukumo ambao utanifanya nifike mahali ninapoenda kwa kasi na haraka. Mambo yote yanafanya kazi kwa faida yangu! Utukufu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 19:26

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 8-10



**2 Wafalme 2:11**
**Ikawa walipokuwa wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto na farasi wa moto likawatenga wale wawili, naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli.**

Kabla ya maandiko ya leo, Nabii Eliya alisafiri kutoka Gilgali hadi Betheli hadi Yeriko na hatimaye mpaka Yordani, ambako alienda Mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Alihama kutoka mahali hadi mahali hadi akapata mazingira yanayofaa yaliyojaa kiwango cha mvuto wa kiroho na shughuli ambazo zinaweza kutumika kama mlango wa kuelekea ukanda mwingine wa ulimwengu wa roho. Kuna baadhi ya mazingira ambayo yanakusukuma katika Roho kukamilisha mengi zaidi. Mazingira katika Roho yaliweka ngazi ya kusafirishwa hadi katika kiwango kingine.

Katika mazingira sahihi, miujiza hudhihirishwa, na uponyaji hufanyika. Lazima uelewe mazingira ambayo yanadumishwa na shughuli za kiroho yana uwezekano ambao unaweza kubadilisha hatima yako. Kuna wanadamu ambao pia ni wabeba mazingira ambayo yanaendeleza uwezo wa kubadilisha maisha yako milele. Kazi yako ni kutafuta mazingira haya ambayo unapokutana nayo, akaunti yako ya benki lazima ibadilike, ndoa yako lazima ibadilike, familia yako lazima ibadilike, na ukiyapata, yathamini!

## UKIRI WA KINABII

**Nimeingia katika mazingira sahihi ya kupokea muujiza wangu, na siondoki mtupu. Akili yangu iko macho, na moyo wangu uko tayari kupokea. Maisha yangu lazima yabadilike leo, na nitashuhudia.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**Mwanzo 5:24**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 11-13



**Mathayo 7:25**
**Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile; isianguke, kwa maana misingi yake iliwekwa juu ya mwamba.**

Biblia inasema kulikuwa na mvua, mafuriko, dhoruba na pepo - yote yakiwakilisha purukushani za maisha - yakipiga nyumba. Nyumba inayozungumzwa katika andiko hili ni wewe. Ndio, unayesoma neno hili sasa. Kumbuka, wewe ni hekalu la Mungu, hivyo kila kitu adui anatupia kwako. Huenda huna kazi, na ndoa yako huenda ikakabili changamoto kubwa zaidi kuwahi kutokea. Kama vile kutembea kwenye kamba, haya yote yanaweza kutokea kwa wakati mmoja, lakini usijali!

Dhoruba za maisha zinakuja dhidi yako kwa kusudi moja tu la kuujaribu msingi wako! Habari njema ni kwamba, kama Wakristo, Kristo ndiye msingi wetu. Ikiwa msingi ni Kristo, uwe na uhakika, haujakwama katika tatizo hilo; hayo unayopitia! Husubiri kuona mwanga mwishoni mwa handaki, hapana. Uliingia humo kama nuru, kwa maana wewe ni nuru ya ulimwengu. Jua kwa hakika shida yako ina tarehe ya kuisha, kwa hivyo hutabaki katika hiyo.

## UKIRI WA KINABII

**Ninasimama juu ya mwamba imara ambao ni Kristo. Sijachukuliwa na hali na dhoruba. Bila kujali ukubwa wa dhoruba, sitaanguka, nitabaki nimesimama! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 10:25

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 14-16



**2 Mambo ya Nyakati 20:20**
**Wakaamka asubuhi na mapema, wakaenda nje katika jangwa la Tekoa; nao walipokuwa wakitoka, Yehoshafati akasimama, akasema, Nisikieni, enyi Yuda, nanyi wenyeji wa Yerusalemu; Mwaminini BWANA, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii wake, ndivyo mtavyofanikiwa.**

Tamko hili kuhusu kumwamini Mungu na manabii wake ni msingi katika mafanikio ya maisha. Kiu kuu ya Mungu sio kuvuna nafsi! Lo, mtu fulani ametikiswa huku mfumo wake wote wa imani umekaa katika hili, lakini elewa, kweli haina hisia. Tamaa kuu ya Mungu ni kuaminiwa. Hivyo ndivyo! Badili mtazamo wako, amini, na umchukue Mungu kwa ujasiri katika neno Lake, basi kuimarishwa kwako kutakuwa imara kama msingi thabiti.

La kuvutia ni kwamba, Mungu anaunganisha ustawi wako na kuwaamini manabii wake. Mafanikio ni kazi ya kumwamini nabii wa Mungu. Muhimu ni kwamba Mungu ni Mungu wa utaratibu na kanuni. Amosi 3:7 inasema: "Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." Mungu huheshimu neno Lake na hutufundisha kuelewa kwamba Yeye hufanya kazi katika sayari ya Dunia kupitia msemaji Wake, nabii, na kwa kumwamini tu nabii Wake, usitawi wako umehakikishiwa!

## UKIRI WA KINABII

**Nimewekwa tena ili nitembee katika mafanikio yangu na kuishi maisha yenye ufanisi kama vile ninavyomwamini Nabii wa Mungu. Hakika nimebarikiwa kuwa na nabii. Neno la Mungu haliwezi kusema uongo; katika mwaka huu wa maziwa na asali mafanikio yangu ni sasa! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 38:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 17-20



**Yohana 10:10**
**Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.**

Baadhi ya watu huchukulia huduma ya Neno la Mungu kama kitu kidogo na cha kawaida katika huduma ya kanisa, mhubiri tu anayetoa Neno kama ulivyo utaratibu! Hata hivyo, hii sivyo. Mtu wa Mungu anapotokea kwenye mimbari, kile unachokiona ni cha kimwili, lakini hali halisi katika ulimwengu wa roho ni tofauti! Maneno yanayotolewa kwenye mimbari si maneno matupu na ya kawaida tu, hapana. Ni silaha za moto zinazosababisha uharibifu katika kambi ya adui.

Paulo alisema katika 1 Wakorintho 15:31, "Naam ndugu zangu, kwa huku kujisifu kwangu niliko nako juu yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu, ninakufa kila siku." Paulo anasema uwezekano wa kufa kila siku wakati wa kuhubiri Injili ni mkubwa. Kutumikia Neno la Mungu kunaweza kusababisha kifo, lakini katika ulimwengu wa roho, mapepo wanalia! Hii ni sababu mojawapo inayowafanya wakristo kuwa na wajibu wa kuwaombea watu wa Mungu kila mahali hata iweje. Ajenda ya shetani ni ya uharibifu, na anahitaji kuadhibiwa!

## UKIRI WA KINABII

**Ninainua mikono ya mtu wangu wa Mungu. Ninaungana na mhubiri wangu kumwadhibu shetani; maneno nisemayo ni uzima na ni roho. Adui yuko taabani sasa hivi kwa sababu ninatamka na kuomba! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 7:25

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 21-23



**Mwanzo 26:3**
**Kaa ugenini katika nchi hiyo, nami nitakuwa pamoja nawe, na kukubariki; maana nitakupa wewe na uzao wako nchi hizi zote, nami nitakifanya imara kiapo nilichomwapia Ibrahimu baba yako;**

Inachekesha mtu kusema kwamba Mungu hahusiki na mafanikio! Tunapokiri maisha ya maziwa na asali hawachukulii kwa uzito. Hata hivyo, baadhi ya Wakristo wenye nia njema wanaamini wanapoishi maisha duni, ya omba omba, yanaonyesha uchaji kwa Mungu na kwa kuwa hivyo tiketi yao ya kwenda Mbinguni imekatwa tayari! Hawa ni halisia ambao wamekosea kwa dhati kabisa! Wakristo wengine hata wanaamini kwamba ikiwa unafanikiwa, ni akili yako mwenyewe na ujuzi vinavyokusababisha, lakini Mungu si sehemu ya mlinganyo huo.

Ikiwa wewe ni Mkristo, basi unapaswa kumjua Abrahamu, Baba wa Imani, ambaye Mungu alisema naye wazi wazi akisema, "Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, nami nitakubariki; Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka." (Mwanzo 12:2). Ikiwa unaamini kwamba Mungu alimwambia Ibrahimu maneno haya, basi ujue kwamba Mungu hafurahii umaskini. Badala yake, anafurahia ustawi wa mtumishi wake (Zaburi 35:27). Umebarikiwa kuwa baraka kwa wengi!

## UKIRI WA KINABII

**Mafanikio ni jina langu la ukoo. Mimi ni makao makuu ya Mungu; Siwezi kuishi maisha ya kupungukiwa na uhitaji maana urithi wangu ni wa Mungu. Popote niendapo, nitaendelea kuwa baraka, katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mwanzo 13:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo Kumbukumbu la Torati 24-27



**2 Timotheo 2:15**
**Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.**

Katika siku zetu za awali, niliwahi kuleta nyumbani kitabu nilichonunua kuhusu fedha. Nilimweleza mke wangu jinsi kitabu hiki kingetufanya kuwa matajiri! Nilimwambia tutakuwa na mara milioni ya kile nilichotumia kwenye kitabu kwa kiwango cha maarifa nilichopata kwa kukisoma! Maandiko yanatuambia katika Mithali 4:7, "Hekima ndiyo jambo kuu; basi jipatie hekima; na kwa mapato yako yote jipatie ufahamu." Ni muhimu kwamba usome vitabu na nyenzo nyingine zinazoboresha ukuaji wako wa kiroho na ufahamu.

Baadhi ya Wakristo hupanga foleni kwenye mistari mirefu wakisubiri kununua chupa ya mafuta ya upako badala ya kuwekeza kwenye vitabu na nyenzo nyingine ambazo zitawajengea uwezo na maarifa. Ingawa sipingi mafuta ya upako kama mfereji wa upako, maarifa yanayopatikana kupitia vitabu yamefungashwa na kuongeza ufahamu wako wa jinsi bora ya kuzunguka maisha na kushinda. Usipuuze kusoma Neno la Mungu na nyenzo zingine za kiroho kwa mbadala wa chupa ya upako. Kila kimoja kina jukumu lake la kukujenga kwa ajili ya maendeleo ya Ufalme.

## UKIRI WA KINABII

**Nimejengwa ili kuyateka mataifa kupitia maarifa. Mimi sio kawaida; Nina hekima kutoka juu. Neno la Mungu ndani yangu hunipa ufahamu wa kukabiliana na changamoto za maisha. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 28-29



**Isaya 54:2**
**Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako...**

Wakati mwingine, unahitaji kuwa mjamzito wa kitu kipya ili kubadilisha hamu yako. Ikiwa hakuna jipya la kukusukuma nje ya eneo lako la faraja, tarajia hakuna jipya litakalotokea. Mwanamke anapokuwa mjamzito, kuna mabadiliko fulani katika hamu yake ambayo huwa hayajitokezi hadi anapokuwa mjamzito. Hili likitokea, elewa kuwa sio mwanamke anayedai chakula kipya, mtindo mpya wa mavazi, malazi mapya, usalama mpya wa kifedha, hapana. Kuna kitu kinasukuma mahitaji hayo, na hiyo ndiyo mimba!

Wakati mazingira yako yanaonekana kukusumbua kwa ghafla, gari lako halikutoshi tena, kabati lako la nguo limekuwa dogo, namna yako ya mavazi inadai uboreshaji, n.k., basi ujue ni wakati wa maziwa na asali!. Mungu anapokuhamisha kwenye mwelekeo mwingine, msimamo wako wa sasa unakuwa hauridhishi, na mwendo wa mabadiliko unakuwa usioweza kurudi nyuma. Msukumo kutoka ndani sio wa kwako mwenyewe bali ni wito kutoka kwa ujauzito ili kupanua upeo wako na kuzaliwa kitu kipya ambacho kitakuwa baraka kwa vizazi vijavyo!

## UKIRI WA KINABII

**Niko tayari, nimewashwa moto kufanya mambo kwa ajili ya Mungu. Ninazalisha kitu kipya ambacho kitashangaza kizazi changu. Nina wito wa kutoka juu na nimewekwa kuteka maeneo mapya kwa ajili ya Yesu! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 26:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 30-31



**Zaburi 41:9**
**Msiri wangu tena niliyemtumaini, aliyekula chakula changu, ameniinulia kisigino chake**

Changamoto nyingi za maisha hutoka kwa vyanzo visivyotarajiwa. Daudi aliomboleza katika andiko hapo juu kuhusu chanzo cha matatizo yake: marafiki walioshiriki mkate na kula naye. Mwishowe, yule ambaye Daudi alimwaona kuwa "rafiki" aliinua kisigino chake dhidi yake! Rafiki huyu alikuwa amekuwa na kiburi na majivuno na kujiona kuwa mkubwa sana wakati, kwa kweli, hakuwa kitu. Usaliti mbaya zaidi mtu anaweza kufanyiwa ni kutoka kwa wale anaowaona kuwa marafiki ilihali wanakuchoma kisu mgongoni.

Nimehitimisha kuwa maisha ni mlipuko usio na marafiki. Baadhi ya marafiki ni maadui wa baadae! Wengine watasema yeye ni rafiki yangu mwandani, lakini miaka miwili baadaye, wanakuwa adui yako mbaya zaidi! Chunguza mahusiano yako ili uweze kutofautisha wale ambao watabaki na wewe katika hali ngumu na mbaya. Nakuombea leo Mungu akupe utambuzi wa kuwagundua haraka watu hao waliokuzunguka, iwe wapo kwa sababu itakayowafanya washikamane nawe, au kwa muda tu, waondoke haraka bila kusababisha madhara kwenye hatima yako. .

## UKIRI WA KINABII

**Nimezungukwa na malaika. Udanganyifu wowote wa adui anayejifanya rafiki hautadumu! Nimekingwa katika neema ya Mungu; maisha yangu yamelindwa katika Kristo! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 22:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Kumbukumbu la Torati 32-34, Zaburi 91



**1 Wakorintho 12:10**
**na mwingine matendo ya miujiza; kwa mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha;**

Wakristo wanaoishi katika kipindi hiki ni bora zaidi na dhaifu zaidi. Tumepewa silaha bora zaidi ambazo Mungu anazo katika ghala lake la silaha, karama zinagawanywa, lakini kushindwa kwetu kutumia silaha hizo kunasababisha tuishi maisha ya unyonge na kushindwa! Tunapaswa kuwa wenye nguvu zaidi, lakini kwa masikitiko makubwa, Ukristo umepunguzwa hadi kuwa itikadi. Ni wakati ambapo Wakristo wanapaswa kutumia sauti na nyuzi za sauti za malaika mkuu kutengeneza data sahihi ili kuunda msimbo ambao utazalisha udhihirisho wa muujiza!

Wakati fulani, Wakristo huomba kwa saa nyingi. Hata hivyo, bili zao hubakia bila kulipwa, ukosefu wa ajira unaendelea kudumu, na hata usaidizi wa kifedha kwa kazi ya Mungu unakuwa hiari na chaguo! Nguvu ya kumiliki tayari iko ndani yako. Kinachokosekana ni muunganiko wa kanuni sahihi za kutoa matokeo. Lisha Neno na weka kipimo cha maombi, pamoja na kufunga ili kuuvunja mwili na kuwa makini kwa Roho Mtakatifu. Kisha, unapoamuru kwa sauti ya malaika mkuu, maombi yako hayatakataliwa kamwe

## UKIRI WA KINABII

**Ninanena roho; Ninatamka maziwa na asali; Ninatamka uzima. Usikivu wangu katika ulimwengu wa kiroho unainuliwa hadi viwango bora zaidi. Vitu vya kiroho ninavyoamuru na kutangaza vitadhihirika kwa utukufu wa Mungu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 16:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 1-4



**Mhubiri 10:19**
**Karamu hufanywa kwa ajili ya kicheko, na divai huyafurahisha maisha; na fedha huleta jawabu la mambo yote**

Neno la Mungu linasema kwa mkazo kwamba huwezi kutumikia mabwana wawili; utakuwa mwaminifu zaidi kwa mmoja na kutokuwa mwaminifu kwa mwingine. Mungu huweka pesa kwenye mabano ya bwana, mungu, ambayo ina maana kwamba pesa hutawala. Ukielewa Mungu anakukabidhi pesa kama wakili, msimamizi; pale Bwana aliyekupa akihitaji kuzitumia kwa makusudi yake, hautasita.

Zingatia: pesa ni kitu katika ulimwengu wa kiroho. Pesa kwenye mkoba wako au pochi haina ufahamu kuwa ni yako. Pesa ina kiburi, kwa hivyo pesa inaweza kudhibitiwa tu na bwana! Pesa ni kitu cha kiroho, na inataka kuabudiwa! Kupenda pesa ni chanzo cha maovu yote, hivyo elewa upendo wako unapoelekezwa kwa Mungu, kila ulichonacho kitakuwa kwa ajili yake, ikiwa ni pamoja na fedha zako. Haitakutawala! Pesa inapojua ulimpa bwana mwingine - Mungu - itakuheshimu na kuvutiwa kwako!

## UKIRI WA KINABII

**Ninajua sasa cha kufanya na pesa; haitanitawala. Nitakabidhi pesa kama mateka kwa Bwana wangu Yesu. Ninapotamka, pesa hunitii na kuzalisha maziwa na asali kwa Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 6:24

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 5-8



**Isaya 43:1**
**Lakini sasa, BWANA, aliyekuhuluku, Ee Yakobo, yeye aliyekuumba, Ee Israeli, asema hivi, Usiogope; maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako; wewe u wangu.**

Hatima inapoita, huna maelezo ya uhalisia fulani wa maisha yako mwenyewe. Unaweza kujipata katika huduma na usiweze kueleza kimantiki kwa nini uko hapo. Biblia inasema Yohana Mbatizaji alikuwa jangwani. Hakukuwa na Instagram, WhatsApp, YouTube, au televisheni. Hata hivyo, sauti ya Yohana ilisikika nyikani, na watu kutoka jijini wakamiminika ili kusikiliza mafundisho yake. Hatima inapoita, umbali sio kizuizi, mazingira ya kijiografia hayazingatiwi, na utabaka wa kijamii hauhesabiwi.

Kitu pekee ambacho husikika katika roho yako wakati hatima inaita ni sauti ya yule ambaye ameletwa kwako. Mungu huwatumia wanadamu kubadili hatima, hivyo ni muhimu kujua Mungu amemweka nani katika maisha yako ili kubadilisha hatima yako. Mungu hayupo kuleta maana; yupo kuifanya imani. Mungu anapokaribia kukubariki, anakutumia mtu, na ni jukumu lako kumjua huyo mtu ni nani. Mungu alikuita kwa sababu. Chukulia wito wako kwa uzito; ni hatima inaita!

## UKIRI WA KINABII

**Hatima yangu inajitokeza. Ninajua nimechaguliwa kutangaza Habari Njema ya neema ya Mungu kwa kipindi hiki cha mwisho kwa kibali na bila woga. Haleluya. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 100:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 9-11



**1 Yohana 2:17**
**Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake; bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.**

Ziada na maisha zaidi ya kawaida huchukuliwa kuwa maisha ya baada ya anasa. Watu ulimwenguni ambao wanachukuliwa kuwa matajiri wanaishi maisha ya baada ya anasa, lakini wanakula mboga na matunda na hawasumbuki kuvaa nembo za bei ghali zaidi. Maisha ya baada ya anasa hayapimi wala kunuia kuishi kama mtu mwingine. Hujui mitego, heka heka za mtu ambaye "amefika" maishani, kwa nini ujaribu sana kuiga maisha yao?

Iga ya kiroho, si ya kimwili. Ujana unaweza kukupofusha, na mitazamo inaweza kuwa inakutawanya, kwa hivyo unakosa maongozi ya Roho Mtakatifu. Jifunze kuishi maisha yanayoongozwa na Roho, ambayo ni maisha ya baada ya anasa. Usiende kwenye yale mambo ambayo yana mwelekeo wa kukuangamiza. Wewe ni jenerali kwa muundo, kwa hivyo usishinikizwe na watu, jamii, au vikundi rika. Wewe ni mtoto wa Mfalme, kwa hivyo utajiri, heshima, umaarufu na ustawi ni mali yako! Umekusudiwa ukuu na hakika utakuwa na tija na matunda!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi zaidi na juu ya hali. Mimi ni chanzo cha msaada kwa taasisi na mataifa. Ninaishi maisha ya neema tele, asante Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 7:31

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 12-15



**1 Timotheo 6:16**
**Amekaa katika nuru isiyoweza kuharibiwa,wala hakuna mwanadamu aliyemwona,wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye milele. Amina.**

Biblia inapozungumza juu ya ' mkono wa Bwana ' au ' kidole cha Mungu ', hairejelei mikono halisi au vidole bali kizio cha Mungu. Waefeso 4:10 inasema, "Yeye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa juu sana kuliko mbingu zote, ili avijaze vitu vyote." Pia, Mwanzo 1:1 inatangaza, "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi." Ikiwa Mungu anaweza kuumba mbingu, ina maana hayupo hapo!

Mungu alipaa juu zaidi ya mbingu zote: iwe mbingu ya pili au ya tatu, Mungu alipaa juu ya zote! Biblia inatangaza kwamba mbingu za mbingu haziwezi kumtosha Mungu! Mungu ni mkubwa sana kwa Mbingu kumtosha! Wengine wanaweza kusema tunamwona Mungu anakaa Mbinguni. Hata hivyo, Biblia inasema kwa mkazo kwamba Mungu anakaa katika nuru ambayo hakuna mwanadamu anayeweza kuikaribia! Unachokiona ni akisi ya Mungu aliye Mbinguni. Vito vya thamani kama yaspi na yakuti vinavyounda kiti cha enzi cha Mungu vyote huangazia nuru. Mungu huelekeza nuru yake kwenye kiti cha enzi, si Yeye anayeonekana.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatembea katika nuru ya Mungu. Sitaogopa, kwa maana Neno la Mungu ni taa ya miguu yangu na mwangaza wa njia yangu. Giza halina nguvu juu yangu kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 1:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 16-18



**Mithali 11:30**
**Mazao ya mwenye haki ni mti wa uzima; na mwenye Hekima huvuta roho za watu.**

Kuvuna nafsi ni uwekezaji wa umuhimu wa milele ambao Kanisa linahitaji kufahamu. Ulimwengu utafanya mengi kwa ajili ya uwongo kuliko Kanisa lilivyo tayari kufanya kwa ajili ya ukweli. Mtindo unayovuma unapotangazwa, watu ulimwenguni watakimbilia kana kwamba hiyo ndiyo maisha yote. Kila mtu huko nje atafuata kwa upofu na kujiweka chini ya chochote ambacho ulimwengu wa mitindo umeweka juu yao bila hata kusita au pingamizi lolote la kukivaa! Kwa nini? Kwa sababu ni ukisasa kuonekana hivyo!

Mkasa wa yote ni kwamba hii imeingia ndani ya Kanisa bila kujua na inapigiwa makofi. Hatuangalii tu kwa mbali; tumejiunga na kuitangaza. Tumetengwa (watakatifu) na kuitwa kuwa wavuna nafsi wenye ufanisi, lakini mpaka tutakapoita dhambi kama jinsi ilivyo, hatuwezi kuwa wavuna nafsi wenye ufanisi. Ili kuwa wavuna nafsi mwenye ufanisi, lazima uone na kutambua hatari. Lengo lako kama wavuna nafsi ni kumtoa mtu huyo kutoka Kuzimu hadi Mbinguni! Elewa leo kwamba umezaliwa ili kuvuna nafsi!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaenda eneo langu, mahali nilipopangiwa kazi, ili kuvuna nafsi kwa ajili ya Yesu! Ninaelewa wajibu wangu kikamilifu sasa; kazi yangu ya wakati wote ni kuvuna nafsi sasa na siku zote. Utukufu ni kwa Mungu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 5:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 19-21



**Luka 10:19**
**Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.**

Mtu anaweza kuwa mfupi, mdogo, mrefu, au chochote unachoweza kuona kama wastani, lakini hiyo ni kawaida. Walakini, nguvu ni kamili! Hakuna mashindano au mabishano wakati nguvu imedhihirishwa. Katika nyakati hizi za mwisho, tunahitaji nguvu ya Mungu ionekane ambayo itaondoa mabishano na falsafa zisizo na maana. Kanisa la leo linapaswa kuwa kielelezo cha nguvu kwa wote kuona kwamba Yesu ni Bwana.

Je, mizunguko yako ya matatizo yasiyoisha inaweza kutokea kwa sababu ya kushindwa kwako kutumia mamlaka yako? Je, inawezekana kwamba adui aliamua kukupa changamoto kwa makusudi kwa sababu hujajitambua wewe ni nani? Nafasi yako katika Kristo imesisitizwa katika Waefeso 5:30: "Kwa maana sisi tu viungo vya mwili wake,". Acha hii izame ndani yako vizuri sana. Unapotembea, Yesu anatembea; unapozungumza maziwa na asali, Yesu anazungumza pia. Maisha unayoishi sasa ni katika Kristo. Kristo ndani yako, tumaini la utukufu!

## UKIRI WA KINABII

**Nina uwezo wa kushinda vizuizi vinavyonijia. Siogopi; Mimi ni jitu katika ulimwengu wa Roho. Ninaposonga, Kristo anasonga. Maisha yangu ni maisha bora! Amina!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 16:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Yoshua 22-24



**1 Samweli 9:3**
**Na punda za Kishi, baba yake Sauli, walikuwa wamepotea. Kishi akamwambia Sauli mwanawe, Haya basi, twaa watumishi mmoja pamoja nawe, uondoke, uende ukawatafute punda hao.**

Katika Israeli, punda huwakilisha ufalme usio na mwisho. Ndiyo maana Yesu alipanda punda wakati wa kuingia kwake kwa ushindi Yerusalemu. Unaposoma zaidi katika hadithi yetu ya maandiko, Sauli hatimaye alitiwa mafuta na Nabii Samweli kama mfalme wa kwanza wa Israeli. Ilichukua hali ya kupotea punda kwa Sauli kuhamia kwenye hatima yake kuwa mfalme juu ya Israeli. Tatizo ambalo lilizuka bila kutarajiwa katika biashara na familia yako ni mpango wa kupanua himaya yako ya kifedha.

Kila kitu kinachojaribu kukuangamiza, tunapomaliza mwezi huu, tunakomesha. Acha chochote kinachokosekana katika maisha yako kipatikane sasa kwa Jina la Yesu! Hakutakuwa na kuchelewa tena kwa ushuhuda wako wa maziwa na asali! Vilio vimeondolewa katika maisha yako, na leo ni alama ya mwanzo mpya. Wamisri unaowaona leo, hutawaona tena! Acha mfalme ndani yako asimame kwenye hafla hiyo. Ushuhuda wako utakuwa wa hakika, na uzuri wa kiwango chako kinachofuata utakuwa wazi kwa wote kuona.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa kutawala; hakuna shida itanishusha. Ninaishi maisha ya ushindi! Kutoka kwangu na kuingia kwangu kutabarikiwa. Mimi ni mbeba HabariNjema! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waamuzi 5:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Waamuzi 1-2



**Ufunuo 2:4**
**Lakini, nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.**

Unapotaka kweli KUWAKA kwa ajili ya Mungu, lazima utengeneze njaa. Ni ndani ya njaa iliyoumbwa ambamo moto huanza kuwaka kutoka ndani. Wakati kuna njaa, unakuwa makini kwa maongozi ya Roho Mtakatifu. Ukikaa peke yako katika chumba chako, mzigo unakuja kwa namna ya maagizo kwa ajili ya huduma. Hata hivyo, kama huwaki, unaweza kupuuza kile Roho Mtakatifu alichokuambia na kutokichukulia kwa uzito, na kuahirisha. Roho Mtakatifu anazungumza nawe waziwazi, lakini bila njaa, huwezi kuwasha moto!

Wanaume na wanawake waliojawa na njaa watatumiwa na Mungu. Wanathubutu kupinga taratibu na kubaki waaminifu kwa Mungu wao wakati wa magumu! Watakuwa kama wale wavulana watatu wa Kiebrania waliosema, 'Ee mfalme, hatutaisujudia sanamu ya dhahabu, ikiwa Mungu hatatuokoa katika jambo hili, hatutashindwa na shinikizo la ulimwengu; na ingawa maisha yetu yako hatarini, hatuna neno katika jambo hili , na Mungu alishuka kwa ajili yao. Acha njaa yako ya mambo ya Mungu ikue, na maisha yako yatakuwa tafsiri kamili ya MAZIWA NA ASALI!


## UKIRI WA KINABII

**Nina njaa ya kuwafunza mataifa. Sina chaguo ila kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu mara moja na bila kukawia. Ninawaka moto, Bwana asifiwe! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 24:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako kwa ajili ya leo: Waamuzi 3-5

GoodNews DAILY




**SUBSCRIBE TO OUR YOUTUBE CHANNEL**

WWW.GOODNEWSWORLD.COM/GOODNEWSDAILY


Become a
GoodNews
DAILY
PARTNER
PARTNER NOW AND HELP SPREAD
THE GOODNEWS AROUND THE WORLD
VISIT www.goodnewsworld.com/ gndpartner

# AYA YA MAANDIKO KWA AJILI YA ULINZI

ISAYA 54.

14: NIMEJENGWA IMARA, NIKATHIBITIKA KATIKA HAKI. MBALI NA SHIDA YOYOTE--HAKUNA CHA KUOGOPA! MBALI NA HOFU-_HATA HAITANIKARIBIA!

15: MTU YEYOTE AKINISHAMBULIA, HATA SITAFIKIRI KWAMBA MUNGU AMEMTUMA. NA IKIWA YEYOTE ATANISHAMBULIA, HAKUNA LITALOTOKEA.

16 MUNGU ALIMUUMBA MUHUNZI AFUKUTAYE MOTO WA MAKAA NA KUFUA SILAHA ILIYOUNDWA ILI KUUA. PIA ALIMUUMBA MUHARIBU.

17 LAKINI HAKUNA SILAHA INAYOWEZA KUNIDHURU AMBAYO IMEWAHI KUUNDWA. YEYOTE ATAKAYENITUHUMU ATAONDOLEWA KUWA NI MUONGO. MIMI NI MTUMISHI WA MUNGU HIVYO NDIYO NINAYOWEZA KUTARAJIA MUNGU KWAMBA ATAONA ILI KUHAKIKISHA KILA KITU KINAFANYA KAZI KWA AJILI YA MEMA YANGU.

HIKI NDICHO MUNGU ANASEMA KWANGU NA HAKITASHINDWA KWA JINA LA YESU!

TRANSLATED FROM THE MESSAGE BIBLE IN ENGLISH



## JE, UMESHAMPOKEA YESU KRISTO?

## TUNA KUKARIBISHA KUMPOKEA YESU KRISTO BWANA WA MAISHA YAKO KWA KUOMBA MAOMBI HAYA;

"EE BWANA MUNGU, NINAKUJA KWAKO KATIKA JINA LA YESU KRISTO. NINAAMINI KWA MOYO WANGU WOTE KATIKA YESU KRISTO, MWANA WA MUNGU ALIYE HAI, NINAAMINI KWAMBA ALIKUFA KWA AJILI YANGU NA MUNGU ALIMFUFUA KUTOKA KWA WAFU. NINAAMINI YUKO HAI LEO.NINAKIRI KWA KINYWA CHANGU KWAMBA YESU KRISTO NDIYE BWANA WA MAISHA YANGU KUANZIA LEO, KUPITIA YEYE NA KATIKA JINA LAKE NINAO UZIMA WA MILELE; NIMEZALIWA MARA YA PILI. ASANTE BWANA KWA KUOKOA ROHO YANGU! MIMI SASA NI MTOTO WA MUNGU. HALELUYA"

HONGERA SANA SASA WEWE NI MTOTO WA MUNGU.

---

TO RECEIVE MORE INFORMATION ON HOW YOU CAN GROW AS A CHRISTIAN PLEASE GET IN TOUCH WITH US ON:

UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209

WWW.UEBERTANGEL.ORG | WWW.GOODNEWSWORLD.COM

TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209

www.goodnewsworld.com